

**MADA: CHANGAMOTO NA MBINU ZA KIISIMU KATIKA UFUNDISHAJI
WA STADI YA MAZUNGUMZO KWA WANAFUNZI WA ELIMU YA AWALI**

LAILA HEMED ALI

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA, IKIWA NI SEHEMU YA MASHARTI YA
KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMLI (M.A. KISWAHILI) YA CHUO**

KIKUU HURIA CHA TANZANIA

2015

UTHIBITISHO

Aliyetia sahihi hapa chini anathibisha kuwa amesoma tasnifu hii iitwayo “Changamoto na mbinu za kiisimu katika ufundishaji wa stadi ya mazungumzo kwa wanafunzi wa elimu ya awali” na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya shahada ya uzamili katika Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Dr Nestory Ligembe
(Msimamizi)

Tarehe

HAKIMILIKI

Haki zote zimehifadhiwa hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupiga chapa au kutoa baadhi ya maandishi ya kitabu hiki, kwa namna yoyote ile bila ya idhini ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

TAMKO

Mimi, **Laila Hemed Ali**, natamka na nathibitisha kwa seneti ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwamba tasnifu hii kwa ajili ya shahada ya uzamili ya Kiswahili ni kazi yangu halisi na kwamba haijawahi kuwasilishwa pahali pengine kwa lengo la kutunukiwa shahada ya aina hii.

Signature

Tarehe

TABARUKU

Kwa heshima ya mama yangu Bi Luluwa Bint Mohammed, Mwenyezi Mungu
akurehemu na akulaze pahala pema peponi.

SHUKURANI

Kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu na afya na kuniwezesha kuifanya kazi hii, Alhamdulillah, leo hii nimeimaliza.

Shukurani za dhati kabisa zimwendee Dkt Nestory Ligembe, mhadhiri wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kituo cha Geita. Yeye ametumia muda wake mwingi na adhimu katika kusimamia, kupitia, kusahihisha na kutoa msaada wa maelekezo mpaka kazi ikafika katika hatua hii. Ahsante sana.

Pia shukrani zimwendee Dkt P. Lipembe kwa kunifundisha na kunipa maelekezo ya namna ya kufanya utafiti. Miongozo yake ndio ilifanikisha kufanya kazi hii kama ilivyotakiwa.

Katika namna ya pekee, napenda kukishukuru Chuo Kikuu Huria cha Tanzania hasa kitivo cha sanaa na sayansi za jamii kwa kutupa fursa ya kusoma tukiwa hapa Pemba.

Aidha ningependa kumshukuru Mwalimu Bakari Kombo wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kituo cha Pemba kwa kunipa moyo wa kufanya kazi hii na kunihimiza ili niweze kumaliza kwa wakati.

Nitakuwa sikutenda haki ikiwa sitawashukuru wakaguzi wa somo la Kiswahili wa shule za elimu ya awali, mratibu wa kituo cha walimu wa elimu ya awali, walimu wakuu na walimu wa shule za elimu ya awali ambao wameniwezesha kupata taarifa za kazi hii. Pia sikumsahau Afisa Mdhamsini wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Pemba kwa kunipa ruhusa ya kwenda shule na kukusanya taarifa.

IKISIRI

Lengo la kazi hii ilikuwa ni kuchunguza uhusiano uliopo baina ya ufundishaji wa stadi ya mazungumzo kwa wanafunzi wa shule za elimu ya awali kisiwani Pemba na kukwama kwao kupata maarifa ya stadi hiyo vya kutosha. Utafiti huu umefanywa katika wilaya ya Chake Chake, mkoa wa Kusini, Pemba. Washiriki wa utafiti walikuwa ni mratibu wa kituo cha walimu wa elimu ya awali, wakaguzi wa somo la Kiswahili kwa walimu wa elimu ya awali, walimu wakuu na walimu wa elimu ya awali. Matokeo ya utafiti yamebaini kuwa, walimu hawana ujuzi wa kutosha wa kutumia njia za ufundishaji wa stadi ya mazungumzo. Wanafunzi hawajifunzi lugha yao ipasavyo kupitia mazungumzo kutokana na walimu kukosa umahiri katika ufundishaji. Walimu hawatumii zana za kufundishia ipasavyo katika ufundishaji wa stadi ya mazungumzo, hii imewafanya wanafunzi hawa kutojifunza lugha ya mazungumzo kwa umakini. Upungufu wa mafunzo kwa walimu ambayo yangeweza walimu kufundisha kwa ufanisi umedumaza ufundishaji wa stadi ya mazungumzo. Mapendekezo yaliyopendekezwa ni walimu wa shule za awali wa somo la Kiswahili kupatiwa mafunzo yanayohusu ufundishaji wa stadi ya mazungumzo, njia za kufundishia stadi hii pamoja matumizi bora ya zana za kufundishia ili wanafunzi waweze kumudu kufundisha stadi ya mazungumzo. Tafiti nyingine zifanyike katika maeneo mengine ya Zanzibar na Tanzania ili kukuza ufanisi katika ufundishaji wa stadi ya mazungumzo.

YALIYOMO

UTHIBITISHO.....	ii
HAKIMILIKI.....	iii
TAMKO	iv
TABARUKU.....	v
SHUKURANI	vi
IKISIRI	vii
YALIYOMO.....	viii
ORORTHA YA MAJADWALI	xii
VIFUPISHO	xii
SURA YA KWANZA.....	1
1.0 UTANGULIZI.....	1
1.1 Usuli wa Mada.....	1
1.2 Tatizo la Utafiti.....	6
1.3 Malengo ya Utafiti	6
1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti	6
1.3.2 Malengo Mahsusini ya Utafiti	7
1.4 Maswali ya Utafiti	7
1.5 Umuhimu wa Utafiti	8
1.6 Kiunzi cha Nadharia	9
1.7 Mipaka ya Utafiti.....	12
1.8 Vikwazo vya Utafiti na Utatuza wa Vikwazo	12
1.9 Muhutasari	13
SURA YA PILI.....	14

2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI	14
2.1 Mapitio ya Kazi Tangulizi Kinadharia Kuhusu Lugha ya Mazungumzo.....	15
2.2 Njia Zinazotumiwa na Walimu wa Madarasa ya Elimu ya awali katika Kukuza ..	18
2.3 Zana za Kufundishia Stadi ya Mazungumzo Zinazotumiwa na Walimu.	25
2.4 Changamoto Zinazowakabili Walimu katika Ufundishaji wa Stadi ya Mazungumzo	27
2.5 Mapitio ya Kazi Tangulizi za Utafiti Kuhusu njia za Ufundishaji wa Stadi ya Mazungumzo	28
2.6 Mapitio ya Kazi Tangulizi za Utafitikuhusu Zana za Kufundishia Stadi ya Mazungumzo	31
2.7 Mapitio ya Kazi Tangulizi za Utafiti kuhusu Changamoto za Ufundishaji wa Stadi ya Mazungumzo.	32
2.8 Muhutasari	33
SURA YA TATU.....	35
3.0 MBINU ZA UTAFITI	35
3.1 Mkabala wa Utafiti	35
3.2 Eneo lalUtafiti.....	35
3.3 Usampulishaji	37
3.4 Sampuli	37
3.5 Mbinu za Kukusanya Data.....	39
3.5.1 Mbinu Ya Mahojiano.....	40
3.5.2 Mbinu ya Ushuhudiaji	41
3.6 Maadili ya Utafiti.....	42
3.7 Uchambuzi wa Data, Matokeo na Majadiliano ya Matokeo	43

3.8 Muhutasari	44
SURA YA NNE.....	45
4.0 UCHAMBUZI WA DATA, UWASILISHAJI NA MAJADILIANO YA MATOKEO	45
4.1 Utangulizi	45
4.2 Njia Zilizotumika katika Ufundishaji wa Stadi ya Mazungumzo	45
4.2.1 Majadiliano kama Njia ya Kufundishia Stadi ya Mazungumzo.....	48
4.2.2 Njia ya Maswali na Majibu katika Kufundishia Stadi ya Mazungumzo	50
4.2.3 Njia ya Hadithi / Masimulizi Katika Kufundisha Stadi ya Mazungumzo	54
4.2.4 Njia ya Maigizo Katika Kufundishia Stadi ya Mazungumzo.....	57
4.2.5 Michezo na Nyimbo kama Njia ya Kufundishia Stadi ya Mazungumzo.	59
4.2.6 Njia ya Ziara na Uchunguzi katika Kufundisha Stadi ya Mazungumzo	61
4.2.7 Njia ya Bungua Bongo katika Ufundishaji Stadi Yya Mazungumzo kwa Watoto.....	64
4.2.8 Njia ya Vitendawili katika Kufundishia Stadi ya Mazungumzo kwa Watoto	65
4.3 Mahojiano na Walimu Wakuu kuhusu Ufundishaji wa Stadi ya Mazungumzo....	66
4.4 Mahojiano na Wakaguzi wa Elimu ya Awali na Mratibu Wa Kituo Cha Walimu	67
4.5 Zana Za Kufundishia Na Kujifunzia Stadi Ya Mazungumzo.....	68
4.6 Mahojiano na Wakaguzi na Mratibu wa Elimu ya awali Kuhusu Zana za Kufundishia Stadi ya Mazungumzo	70
4.7 Changamoto Wanazokabiliana Nazo Walimu Katika Ufundishaji Wa Stadi Ya Mazungumzo	71
4.8 Muhutasari	72

SURA YA TANO	75
5.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO	75
5.1 Utangulizi	75
5.2 Hitimisho	75
5.3 Mapendekezo.....	76
MAREJEO.....	78
VIAMBATANISHO.....	81

ORORTHA YA MAJADWALI

Jadwali 1 : Aina ya walengwa waliohojiwa katika utafiti.....	37
Jadwali 2 : Shule zilizofanyiwa utafiti (idadi ya walimu ni pamoja na walimu wakuu)	39

VIFUPISHO

NCLRC	National Capital Language Resource Centre
TIE	Tanzania Institute of Education
TZ21	Tanzania 21 st Century
ZMRC	Zanzibar Madrasa Resource Centre

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Sura hii imegawanyika katika sehemu nane. Sehemu ya kwanza ni utangulizi ulioeleza kwa undani kuhusu stadi ya mazungumzo kwa jumla, njia na zana za ufundishaji wake pamoja na changamoto zinazowakabili walimu katika ufundishaji wake. Sehemu ya pili inaeleza tatizo la utafiti ambalo limelenga katika kuchunguza njia, zana pamoja na changamoto wanazokutana nazo walimu katika ufundishaji wa stadi ya mazungumzo.

Sehemu ya tatu imeeleza kuhusu lengo kuu la utafiti pamoja na malengo mahsus ya utafiti. Sehemu ya nne imeeleza maswali yaliyoongoza utafiti na madhumuni ya utafiti. Sehemu ya tano imeeleza umuhimu wa utafiti na jinsi utakavyochangia maarifa mapya katika taaluma ya isimu, kwa walimu, wakaguzi wa elimu pamoja na wakuza mitaala kuhusiana na ufundishaji wa stadi ya mazungumzo. Sehemu sita imeeleza kiunzi cha nadharia ambacho kimetumika katika utafiti. Nadharia ya ufundishaji stadi ya mazungumzo imeelezwa na jinsi ilivyotumika katika utafiti huu. Sehemu ya saba imeeleza mipaka ya utafiti, sehemu ilipofanyika utafiti na aina za walimu pamoja na wakaguzi ambao wametafitiwa. Sehemu ya mwisho imeainisha vikwazo alivyokabiliana navyo mtafiti na jinsi alivyoweza kutatua vikwazo hivyo.

1.1 Usuli wa Mada

Watoto hapa kisiwani Pemba wanapofikia umri wa miaka minne huanza elimu ya awali. Sera ya Elimu Zanzibar (2006) inaeleza wazi kwamba watoto wote wa Zanzibar waliofikia umri wa miaka minne, wanatakiwa kuanza elimu ya awali iwe katika shule za serikali, shule za binafsi au shule za kijamii. Sera hii bado haijatekelezwa kikamilifu

kutokana na mwamko mdogo wa jamii wa elimu katika baadhi ya maeneo, na upungufu wa madarasa kwa baadhi ya maeneo hasa ya mijini

Ufundishaji wa lugha umejikita katika stadi nne za lugha yaani mazungumzo, kusikiliza, kuandika na kusoma. Utafiti huu umejikita zaidi katika kuchunguza ufundishaji wa stadi ya mazungumzo kwa watoto wa shule za awali katika wilaya ya Chake Chake, kisiwani Pemba.

Mawasiliano kwa njia ya lugha mara nyingi ndio humfanya mtu asikilize na au azungumze. Watu wanatumia sana stadi za mazungumzo na kusikiliza katika shughuli zao za kila siku. Stadi ya mazungumzo na kusikiliza huhusisha watu wawili yaani mzungumzaji na msikilizaji au zaidi kwa wakati mmoja (ZMRC 2000). Wote wanatakiwa wazungumze na wasikilize vizuri ili mawasiliano yakamilike. Hivyo ni muhimu kuimarisha ufundishaji wa stadi ya mazungumzo.

Watoto wanapokwenda kwenye shule za awali takriban wote wanakuwa na kiwango cha lugha ambacho kwa uhakika huwawezesha kuwasilisha hisia na mapendekezo yao. Aidha, watoto hujenga maingiliano kati yao, kuuliza maswali na kuzungumza mambo mbalimbali kwa kutumia lugha yao wenyewe. Ni muhimu sana kwa watoto kufundishwa stadi ya mazungumzo kwa kutumia lugha yao ya Kiswahili. Watoto wanapata utambulisho na pia hujisikia raha kutokana na lugha ya jamii yao (ZMRC: 2000).

O'hara (2004) anafafanua kuwa wanafunzi wanapokuzwa katika stadi ya mazungumzo wanajengwa kujimini wakati wa kuzungumza. Aidha kwa kuzungumza wanafunzi

wanaweza kuuliza maswali, kujieleza na kujenga uzoefu juu ya mambo wanayofundishwa. Vilevile wanafunzi hao hukuza ufahamu wao katika mambo mbalimbali na pia huweza kutoa hisia na mawazo yao kutokana na ujuzi walio nao.

Bruce (2005) anaongezea kuwa mazungumzo huwafanya watu kufikiri na kuhisi mambo ya kidhahania na kuwafanya wanafunzi waweze kubuni mazungumzo zaidi, yaani kuwa na umilisi mzuri wa lugha. Kutoweza kuzungumza na kusikiliza kutamfanya mtu awe mpweke na akose fursa ya kuwasiliana na watu wengine. Wanafunzi viziwi wao wanazungumza kwa lugha ya alama ambayo inatambuliwa rasmi. Lugha hii hutumia alama zinazotumia vidole. Wasioona husikiliza na kuzungumza na pia huwasiliana kwa kugusa.

Watoto wanapofikia umri wa miaka minne hufurahia mazungumzo ya lugha yao. Wanapofikia umri wa miaka mitano hufurahia nyimbo, hadithi na mazungumzo ya kufurahisha na kuchekesha.

Mfaume (2013) anakubaliana na wenzake waliotajwa hapo kwa kueleza kuwa lugha ya mazungumzo ni ile inayotolewa waziwazi kwa kutumia mdomo. Mfaume ameeleza sifa za mzungumzaji kuwa anatakiwa afahamu vizuri lugha anayotumia, atumie muwala mzuri katika kuzungumza pia atumie lugha fasaha. Mazungumzo yake yavutie na yasiwachoshe wasikilizaji. Mfaume (keshatajwa) pia anasisitiza kuwa mzungumzaji ashirikiane vyema na anayezungumza naye, kuuliza au kujibu maswali wakati wa mazungumzo ya ana kwa ana. Aidha, ametoa sifa za lugha ya mazungumzo kuwa ni nyepesi, hivyo katika jambo muhimu lugha hiyo huweza kutumika kuwaelezea watu

waziwazi. Mfaume ameongezea kwa kueleza kuwa lugha ya mazungumzo inarahisisha mawasiliano. Mzungumzaji anaweza kuulizwa, kupongezwa, au hata kukosolewa hapo hapo. Mzungumzaji pia anaweza kuzungumza huku anatumia ishara.

Mtandao wa “The Elimu Network Linkedin” (2014) wanaeleza kuwa, kusikiliza na kuzungumza ni stadi za kimsingi na muhimu sana katika kujenga haiba ya mwanafunzi, uwezo wake wa kuwasiliana kuhusiana na watu wengine katika kujiendeleza kielimu. Aidha wamesisitiza kuwa stadi hizi huchangia kuimarisha kusoma na kuandika.

Umilisi wa stadi ya mazungumzo hutegemea mwalimu anavyomshirikisha mwanafunzi katika shughuli za kimaingiliano kama vile mazungumzo, dayalojia, michezo ya lugha na mijadala kwenye miktadha na mazingira yanayoakisi hali halisi.

Ingawa kila mwanafunzi aliye katika shule ya awali anaweza kutumia lugha ya mazungumzo Ili kutimiza lengo fulani, ni dhahiri kuwa si kila mmoja huwa na uwezo wa kutumia lugha kwa masharti yote yaliyowekwa na jamii. Uwezo wa kutumia lugha hasa ya mazungumzo hutokana na mazoezi wanayopewa wanafunzi wakati wa kufundishwa kwa kiwango cha uwezo wa akili.

Kazi nyingi zimefanywa kuhusiana na ufundishaji wa stadi ya kusoma na kuandika hasa katika ngazi ya elimu ya msingi lakini si stadi ya mazungumzo na kusikiliza (Wizara ya Elimu 2008; TZ21 2010). Kazi hizi pia hazikuangalia madarasa ya awali. Msingi wa elimu unaanza katika madarasa ya elimu ya awali. Wanafunzi wanapotoka shule za awali na kwenda shule za msingi huwa wanashindwa kujieleza vizuri hasa wanapopatwa

na matatizo kama vile kuchelewa kuja kuchukuliwa na wazazi wao wakati wa kuondoka shule, kupoteza vifaa vyao na hata kunyang'anywa madaftari yao na wenzao wakubwa. Wanafunzi hawa wanakuwa na uwezo mdogo wa kufafanua mambo ambayo wanafundishwa darasani. Wakati mwingine wanashindwa hata kuwakabili walimu wao kuwaeleza shida zao kama vile ugonjwa, kupigwa na wenzao na mengine mengi.

Ufundishaji wa stadi ya mazungumzo haukutiliwa maanani sana kwani walimu hufikiria kuwa mtu anajua tu kuzungumza kwa kuwa ni jambo la maumbile. Watoto wanapewa fursa ya kusimulia hadithi, kutega na kutegua vitendawili pamoja na kuimba nyimbo kama ndio njia za kukuza stadi ya mazungumzo. Walimu hawashughuliki kuandaa vitendo vya ufundishaji ili watoto wakuze stadi hii. Wakaguzi wa elimu wanapokwenda shuleni hawakagui stadi ya mazungumzo inavyofundishwa. Wao hujikita zaidi katika stadi ya kuandika na stadi ya kusoma. Mihutasari ya elimu ya awali (2005; 2010) pamoja na mwongozo wa kufundisha elimu ya awali (2010) kwa somo la Kiswahili imetaja vitendo vya ufundishaji stadi ya mazungumzo kuwa ni pamoja na kuzungumzia picha, habari fupi na pahali mtoto anapoishi. Aidha kusimulia hadithi, nyimbo, vitendawili, ngonjera na mashairi. Hapa tujiulize maswali, je hadithi, nyimbo na vitendawili vinatosha katika kukuza stadi hii? Watoto wasio na uwezo wa kusimulia hadithi, kutega na kutegua vitendawili wanakuzae stadi hii? Mitaala ya elimu ya awali inatoa fursa ya kutosha ya kukuza stadi hii?

Utafiti huu ulikusudia kuchunguza uhusiano uliopo baina ya ufundishaji wa stadi ya mazungumzo na kukwama kwa wanafunzi wa shule za elimu ya awali kupata maarifa ya kutosha ya stadi hiyo ili waweze kujieleza kwa ufanisi kwa njia ya mazungumzo

kisiwani Pemba. Je mambo yapi yanayosababisha wanafunzi hawa washindwe kujieleza vizuri kwa njia ya mazungumzo? Baadhi ya maswali yanayoambatana na kukwama huko kwa watoto kujieleza kwa ufanisi ni kama vile; Kwa nini hawa wanafunzi washindwe kujieleza vizuri kwa njia ya mazungumzo? Je, walimu wanaelewa umuhimu wa stadi ya mazungumzo kwa wanafunzi? Walimu wa shule za awali wana maarifa ya kutosha ya stadi hii ya mazungumzo?

1.2 Tatizo la Utafiti

Utafiti huu ulichunguza kwa nini wanafunzi humaliza elimu ya shule ya awali bila ya kuwa na maarifa ya kutosha ya kujieleza vema kwa lugha ya mazungumzo. Utafiti ulilenga kuchunguza njia za kufundishia stadi hii katika kiwango hiki cha elimu ya awali kama zinatumika ipasavyo ama la. Aidha, utafiti ulichunguza zana mbalimbali za kufundishia namna zinavyotumiwa na walimu katika kuwakuza watoto kwenye stadi ya mazungumzo kama zinatumika ipasavyo ama la. Pamoja na hayo, utafiti ulijadili changamoto zinazowakibili walimu katika ufundishaji wa stadi ya mazungumzo ili kukuza lugha.

1.3 Malengo ya Utafiti

1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti

Adam (2008) anaeleza kuwa malengo ya utafiti ni yale madhumuni yaliyokusudiwa na mtafiti. Malengo hutueleza mtafiti anataka kupata nini mwisho wa utafiti wake. Hivyo basi, lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuchunguza uhusiano uliopo baina ya ufundishaji wa stadi ya mazungumzo kwa wanafunzi wa shule za elimu ya awali kisiwani Pemba na kukwama kwao kupata maarifa ya stadi hiyo vya kutosha.

1.3.2 Malengo Mahsusni ya Utafiti

Malengo mahsusni ya utafiti huu yalikuwa;

- a) Kubainisha njia zinazotumiwa na walimu wa madarasa ya elimu ya awali katika ufundishaji wa stadi ya mazungumzo.
- b) Kubainisha zana mbalimbali za kufundishia zinavyotumiwa na walimu ili kukuza stadi ya mazungumzo kwa wanafunzi.
- c) Kujadili changamoto zinazowakabili walimu katika kufundisha stadi hii ya mazungumzo.

1.4 Maswali ya Utafiti

Andrews (2003) anafafanua kuwa maswali ya utafiti hutokana na malengo ya utafiti.

Maandalizi ya malengo haya ni kazi inayohitaji muda wa kutosha, kwa sababu ndio dira ya kufanya utafiti. Majibu ya maswali ya utafiti yanatakiwa yaongeze maarifa katika taaluma inayofanyiwa utafiti.

Utafiti huu utaongozwa na maswali yafuatayo:

- a) Walimu wa Kiswahili hutumia njia zipi za kufundishia wanapofundisha wanafunzi wa darasa la elimu ya awali stadi ya mazungumzo?
- b) Walimu wa Kiswahili hutumia zana zipi za kufundishia wanapofundisha wanafunzi wa darasa la elimu ya awali stadi ya mazungumzo?

- c) Walimu wa Kiswahili hukabiliwa na changamoto zipi wanapofundisha wanafunzi wa darasa la elimu ya awali stadi ya mazungumzo?

1.5 Umuhimu wa Utafiti

Hapa Zanzibar hakuna tafiti nyingi zilizofanywa kuhusiana na ufundishaji wa stadi ya mazungumzo katika shule za awali. Kazi zilizofanywa na wanazuoni mbalimbali zimechunguza tu uandikishaji wa watoto (Wizara ya Elimu Zanzibar). Kazi zingine chache sana zinahusu stadi ya kusoma (**TZ21** 2010). **TZ21** (keshatajwa) waliangalia ufundishaji wa kusoma kwa madarasa ya awali. Waligundua kuwa walimu wanatumia silabi katika kufundisha kusoma badala ya kutumia sauti za lugha.

Kazi nyingine zilizofanywa ni za kuchunguza uandikishaji wa watoto, matumizi ya mihutasari na ufundishaji wa somo la hisabati na kiingereza (Wizara ya Elimu 2009; 2011; 2013).

Hivyo basi, umuhimu wa utafiti huu ni kama ifuatavyo:

- a) Utachangia maarifa mapya katika taaluma ya isimujamii kwa kuelewa jinsi ufundishaji wa stadi ya mazungumzo unavyofanyika katika ngazi ya elimu ya awali.
- b) Utasaidia wizara ya elimu na hasa wakuza mitaala wa elimu ya awali kuelewa namna ya kutayarisha zana, kuandaa vitabu vya kufundishia pamoja na vifaa ambavyo vitasaidia kukuza lugha ya mazungumzo.
- c) Utafiti huu pia utasaidia wataalamu wa lugha hasa katika taaluma ya isimijamii kuangalia mapengo ya utafiti na wao kuendelea na tafiti nyingine.

- d) Utawasaidia walimu wa lugha kubaini na kutumia njia mbalimbali za kufundishia stadi ya mazungumzo.

1.6 Kiunzi cha Nadharia

Nadharia kama inavyoelezwa na Massamba (2004) ni taratibu, kanuni na misingi ambayo imejengwa katika muundo wa kimawazo kwa madhumuni ya kutumiwa kama kiolezo cha kuelezea jambo. Kiunzi cha nadharia ambacho kimetumika katika utafiti huu ni nadharia ya ufundishaji stadi ya mazungumzo.

Nadharia ya ufundishaji stadi ya mazungumzo

Nadharia hii iliibuka katika miaka ya 1980 na imekubalika katika nchi nyingi duniani. Wanaisimu kama vile Firth (1970, Halliday (1978), na Hymes (1971) walikuwa wa mwanzo kueleza kuwa kujifunza lugha ndio kuwasiliana. (Savignon, S. Communicative Language Teaching).

Tangu siku ya kwanza mtoto anapokuja shule jitihada za mawasiliano zifanyike katika ufundishaaji ili mtoto aweze kumudu lugha. Mwalimu amfundishe mwanafunzi si katika umilisi wa sarufi tu, bali pia katika stadi za jamii yaani nini cha kuzungumza, namna ya kuzungumza, lini mzungumzaji anazungumza na wapi azumngumze lipi ili kuridhisha mahitaji yake ya kila siku.

Kwa upande wa mwalimu, lengo ni kuandaa vitendo ambavyo vitamwezesha mwanafunzi kupata umilisi wa mawasiliano ambayo ni pamoja na umilisi wa kisarufi, umilisi wa uzungumzaji na umilisi wa kiisimujamii kama vile wapi pa kuzungumza, nini cha kuzungumza na nani azungumze nae.

Kwa mujibu wa Firth (1970), nadharia hii pia imetaja misingi ya utumiaji wa lugha ya mazungumzo kama vile;

- a) Namna ya kutumia lugha ya mazungumzo.
- b) Mwalimu afundishe stadi ya mazungumzo katika muktadha halisi wenyewe uasilia.
- c) Ufundishaji wa stadi ya mazungumzo uwe katika hali halisi ya maisha ili mtoto aelewé uhalisia wa maisha.
- d) Ufundishaji wa mazungumzo uwe kama stadi na sio kama somo, mwalimu awafanye wanafunzi wazungumze mambo yanayotokea kila siku katika maisha yao.

Katika ufundishaji wa stadi ya mazungumzo, nadharia hii imetaja mambo ya muhimu kuyazingatia katika muktadha wa ufundishaji (Firth 1970 na Halliday 1978). Baadhi ya hayo ni kama:

- a) Umri wa wanafunzi wanaofundishwa mazungumzo.
- b) Mwalimu anafundisha katika kiwango gani.
- c) Uweledi wa lugha ya mazungumzo ya watoto.
- d) Muktadha wa kijamii

Mwanaisimu Littlewood (1981) katika kuzungumzia nadharia ya ufundishaji wa stadi ya mazungumzo anafafanuaa kuwa, matumizi ya picha katika ufundishaji wa stadi ya mazungumzo ni muhimu sana. Picha zinawavutia na kuwafurahisha wanafunzi hivyo huwafanya wazungumze. Kazi ya mwalimu ni kuyaanzisha hayo mazungumzo kwa kuuliza maswali kuhusiana na hizo picha anazotumia kufundishia. Aidha amezungumzia

michezo ya ndani ya darasa kama vile kuunganisha picha iliyoparaganywa, michezo ya loto, kufananisha picha huwasaidia sana wanafunzi kufanya mazungumzo. Wakati wa ufundishaji, mwalimu awe makini ili michezo isiwachoshe wanafunzi (Littlewood; keshatajwa).

Katika kutilia mkazo nadharia ya ufundishaji wa stadi ya mazungumzo, Intihar (2006) anaeleza kuwa kuchanganya njia tofauti wakati wa ufundishaji wa stadi ya mazungumzo ni kitu cha msingi sana. Wakati wa ufundishaji, mwalimu anaweza kutumia nyimbo anapofanya vitendo vya ufundishaji, michezo na dayalojia. Aidha mwalimu ahakishe anatoa fursa ya kufanya mazungumzo na wanafunzi ili waweze kujifunza misamati mipya, sarufi na matamshi (Intihar: keshatajwa). Mwalimu anapoandaa vitendo hivi, akumbuke uwezo wa wanafunzi wake.

Nadharia ya ufundishaji wa stadi ya mazungumzo inajihuisha na jinsi wanafunzi wanavyofundishwa stadi ya mazungumzo na walimu wanavyofundisha stadi hii ili mwanafunzi apate umilisi wa lugha. Kwa hiyo mtafiti ameona ni vyema kutumia nadharia hii kwa sababu inaendana na kazi ya utafiti huu ambayo ni kuchunguza ufundishaji wa stadi ya mazungumzo katika madarasa elimu ya awali hasa katika vipengele vya njia za kufundishia, zana wanazotumia walimu katika kufundisha stadi ya mazungumzo pamoja na changamoto zinazowakibili walimu katika ufundishaji wa stadi hii.

1.7 Mipaka ya Utafiti

Utafiti ulifanyika katika wilaya ya Chake Chake, mkoa wa Kusini, Pemba. Washiriki wa utafiti walikuwa ni walimu wakuu wa shule husika, walimu wa lugha ya Kiswahili wa madarasa ya awali wa shule husika, wakaguzi wa shule wa masomo ya lugha katika ngazi ya elimu ya awali na mratibu wa kituo cha walimu wa madarasa ya elimu ya awali.

Aidha, utafiti huu umechunguza stadi ya mazungumzo tu, haukuchunguza stadi za kusoma, kuandika na kusikiliza. Mtafiti pia hakuchunguza tathmini ya stadi hii katika elimu ya awali na ufundishaji wa stadi hii kwa wanafunzi wa darasa la kwanza hadi la saba.

1.8 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi wa Vikwazo

Vikwazo ambavyo mtafiti alikabiliana navyo katika utafiti huu ni kama;

Mtafiti alipokwenda katika shule zinazofanyiwa utafiti hasa za serikali, alikuta shule zimefungwa na walimu hawakuwepo. Mtafiti alipanga ratiba yake na kuhakikisha kuwa walimu na wakaguzi wanapatikana. (Angalia kiambatisho cha ratiba).

Wakaguzi walikuwa na kazi za ufuatiliaji wa walimu hivyo upatikanaji wao ukawa ni mgumu. Mtafiti alifanya mawasiliano mazuri na wakaguzi ili kuelewa ni wakati gani wao wanaweza kupatikana. Hivyo wakaguzi hao walipatikana kwenye muda walioupanga.

Walimu walikuwa na ratiba zao za ndani ambazo zimewabana. Mtafiti alifanya mawasiliano mazuri na walimu na kuelewa wakati ambao wanaweza kupatikana. Upatikanaji wa fedha za kufanya utafiti ulikuwa mgumu lakini haukuchelewesha zoezi la ukusanyaji wa data. Mtafiti alitafuta fedha na kupanga bajeti vizuri hivyo alipata fedha za kukamilisha utafiti wake.

1.9 Muhutasari

Katika sura hii vipengele viliwyofafanuliwa ni utangulizi, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti na umuhimu wa utafiti. Aidha, mkabala wa kinadharia, mipaka ya utafiti, vikwazo na utatuvi wake vimejadiliwa.

SURA YA PILI

2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI

Sura hii imeangalia kazi za wataalamu mbalimbali ambao wamezungumzia ufundishaji wa stadi ya mazungumzo kwa watoto wa shule za awali. Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza imejadili mapitio ya kazi tangulizi kidhahania kuhusu lugha ya mazungumzo. Katika sehemu hii imejadiliwa kwa undani kwa kuangalia maoni ya wanadharia mbalimbali katika eneo hili. Baadhi ya mambo yaliyo jadiliwa ni stadi ya mazungumzo kwa jumla, njia na zana mbalimbali na ufundishaji wake, na changamoto zinazowakabili walimu na ufundishaji wake. Sehemu ya pili imejadili tafiti mbalimbali zilizowahi kufanyika kuhusu ufundishaji wa stadi ya mazungumzo. Katika sehemu hii, tafiti zilizowahi kufanyika ndani na nje ya nchi na maeneo ambayo hayakushughulikiwa yamejadiliwa. Sehemu ya tatu ni hitimisho kwa njia ya muhutasari. Katika sehemu hii sura nzima ya pili imeelezwa kwa muhutasari.

2.1.1 Stadi ya Mazungumzo

Stadi ya mazungumzo ni moja kati ya stadi tano za lugha. Stadi zingine za lugha ni kusikiliza, kusoma, kuandika. Mawasiliano ya binadamu hufanywa kwa mazungumzo. Lugha ya kwanza ya binadamu ni lugha ya mazungumzo. Hii ndio njia ya asili, na njia nyingine za mawasiliano kama vile maandishi au ishara ambazo hutumia viungo vya mwili zilifuata. Lugha ya mazungumzo ambayo hutumia maneno ndio inayozingatiwa sana kuliko lugha ya maandishi au ya ishara kwa sababu inatumika zaidi katika mawasiliano ya kila siku. Pia lugha ya mazungumzo hutumiwa na jamii nyingi duniani na hufahamika zaidi na watoto.

Wataalamu wengi kama vile Palmer (1976), Yule (1985) na Meggitt (2000) wameeleza na kufafanua maana, dhima na umuhimu wa lugha ya mazungumzo pamoja na kueleza ufundishaji wa stadi ya mazungumzo.

2.1 Mapitio ya Kazi Tangulizi Kinadharia Kuhusu Lugha ya Mazungumzo

Palmer (1976) anatoa hoja nne kuhusu lugha ya mazungumzo kama ifuatavyo;

- a) Lugha ya mazungumzo ni kongwe kuliko ya kuandikwa, na lugha nyingi zinazungumzwa duniani lakini hazijaandikwa.
- b) Mtoto hujifunza kuzungumza kabla ya kuandika
- c) Mazungumzo yana dhima kubwa katika maisha ya kila siku kuliko maandishi.
- d) Tukichukua lugha ya kuandika na kuigeuza katika mazungumzo hatutapoteza dhana iliyokusudiwa lakini tukiandika kinachozungumzwa tutapoteza mambo mengi.

Hoja hizi za Palmer zinadhihirisha umuhimu wa wanafunzi kuwa na umilisi wa stadi ya mazungumzo. Si wanafunzi wote wenye umilisi huo hivyo ni muhimu wafundishwe stadi hiyo ya mazungumzo.

Mmallavi (1977) anaendelea kufafanua kuwa mazungumzo ndio maana yenyewe ya lugha kwa sababu maneno yake huwa rahisi zaidi kutokana na hali inayosababishwa na mazingira ya wazungumzaji wake. Mambo yanayokamilisha mazungumzo ni pamoja na mikono, uso pamoja na ishara nyingine ambazo hupatikana katika kiwiliwili kizima.

Wakati Palmer (keshatajwa) akitofautisha baina ya lugha ya mazungumzo na ile ya kuandika, Mmallavi (keshatajwa) anasisitiza jinsi ishara za mwili zinazotumiwa wakati mtu anapozungumza zinavyokamilisha mazungumzo hivyo huwezesha mawasiliano fanisi baina ya msemaji na msikilizaji.

Katika kujadili suala la mazungumzo, Yule (1985) anaongezea maelezo kuwa, mtoto anahitaji maingiliano na watumiaji wa lugha ili aweze kujijenga kwenye lugha husika. Ili mtoto aweze kuizungumza lugha ni lazima aisikie lugha hiyo ikizungumzwa vilivyo. Aidha, Yule (keshatajwa) anasisitiza kuwa haitoshi mtoto kusikia sauti za lugha bila kuitumia. Kama mtoto hakusikia lugha ikizungumzwa hatajifunza lugha hiyo. Hii ina maana kuwa lugha ni kitu ambacho mtoto anakipata kutokana na lugha ya mawasiliano mapana katika mazingira anayoishi.

Wakati Yule (keshatajwa) anaelezea mahitaji ya mtoto katika kuingiliana na watumiaji wa lugha, Lyons (1981) anasisitiza zaidi umuhimu wa lugha ya mazungumzo kuliko lugha ya kuandika. Hii inatokana na matumizi ya ishara katika mazungumzo. Lugha ni kitu huru na kitu cha kubadilisha upendavyo wakati wa kuzungumza. Pia Lyons (keshatajwa) anasisitiza kuwa watoto wanajifunza mambo kimaumbile tofauti na kusoma na kuandika ambapo inabidi watoto wapewe ujuzi na kufundishwa stadi hizo.

Meggitt (2000) anaeleza kuwa, watoto wanapokuwa na umri wa miaka 4 - 5 wanapendelea kuzungumza mambo yaliyopita na yajayo. Watoto hawa wanakuwa ni wazungumzaji sana na hupenda kuuliza maswali yanayoanza na kauli za maswali kama vile; kwa nini....? Lini.....? vipi.....? wapi....?

Vilevile watoto hawa huwa wanapenda utani, kutumia maneno mapya ambayo wamejifunza, pia wanapenda kuimba na kusimulia hadithi. Wanapofikia umri wa miaka 5 wanazungumza vizuri na kwa kujiamini zaidi.

Kwa upande wake Whitehead (2002) kama alivyonukuliwa na Bruce (2005) anadai kuwa watoto wenyewe kuzungumza lugha mbili wanakuwa kama wana daraja la kuvuka kutoka lugha yao chanzi kwenda kwenye lugha ya pili. Watoto hawa wanazungumza lugha ya pili kwa kutumia sarufi ya lugha yao ya mwanzo na wanakuwa wanachanganya na kubadili msimbo katika mazungumzo yao.

Beaver (2004) hatofautiani sana na Meggitt anapoeleza kuwa watoto wanapokuwa na umri wa mika 4–5 wanakuwa wanaongeza misamiati ya kuzungumza. Hukuza mazungumzo yao kwa kutoa maeleo na hadithi. Pia hukuza stadi yao ya mazungumzo kwa kuuliza na kujibu maswali. Wakati mwingine wanaweza kufanya makosa ya kisarufi katika mazungumzo, lakini pia huweza kutumia viwakilishi kama mimi, yeye, wao na yule.

Pamoja na hayo, King'ei (2010) anafafanua kuwa si kila mtu ana uwezo wa kutumia lugha kwa masharti yaliyowekwa na jamii. Lugha ya mazungumzo itumiwapo inapaswa kuwa na maana na kutimiza shabaha muhimu iliyokusudiwa kwa mujibu wa utamaduni wa jamii inayohusika. Ili mwanajamii aweze kufanya hivyo, anapaswa kuwa na ujuzi au maarifa sio tu ya lugha yake bali pia kunga za jamii zinazotawala na kuelekeza matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali ya jamii. Uwezo kama huu hutokana na mazoezi ya kujifunza na kiwango cha uwezo wa kiakili wa mtu.

2.2 Njia Zinazotumiwa na Walimu wa Madarasa ya Elimu ya awali katika

Kukuza Stadi ya Mazungumzo.

Suala la ufundishaji wa stadi ya mazungumzo kwa watoto wa shule za awali limejadiliwa na wataalamu wa aina tofauti (Billows, (1966; Goodman, 1977; Burkart, 1998). Billows (1966) anaeleza kuwa wakati wa ufundishaji wa lugha ya mazungumzo, walimu watumie wakati wao kutoa maana ya maneno ikiwa pana umuhimu wa kufanya hivyo. Vitendo vya ufundishaji ambavyo mwalimu atavifanya darasani viwe ni vyenye kusisitiza uzungumzaji. Pia ameeleza kuwa wajibu wa mwalimu ni kutoa fursa kwa watoto kusikia maneno ambayo yanatumiwa ili waweze kugundua mfumo wa sauti unaotumika katika maneno haya.

Kwa upande mwingine Goodman (1977) anaongezea maeleo juu ya stadi ya mazungumzo kuwa, ni vizuri watoto wafundishwe kwa kutumia lugha chanzi wanapokuwa shulenii. Hii itawawezesha kujieleza vizuri juu ya matendo wanayoyafanya na kujiona kuwa ndani ya lugha yao wenyewe. Hivyo basi, ni vema mwalimu aandae vitendo vya ufundishaji ambavyo vitatoa fursa ya maingiliano baina ya wanafunzi.

Billows na Goodman wote wanasisitiza ufundishaji kwa kutumia vitendo vya ufundishaji ambavyo vinatoa fursa ya kuzungumza.

Burkart (1998) anadai kuwa ufundishaji wa lugha ya mazungumzo unachukuliwa kwamba ni uwezo wa kumfundisha mtoto kuzungumza lugha vizuri na ndio kipimo cha kujua lugha vyema. Pia Burkart (keshatajwa) ameendelea kueleza kuwa ufundishaji wa lugha ya mazungumzo una maeneo matatu ya kuzingatia. Eneo la kwanza ni matamshi, yaani huhusisha sarufi na misamiati. Eneo la pili ni uamilifu, yaani kujua kama ujumbe

uliokusudiwa umepatikana, na eneo la mwisho ni kufuata kanuni za mazungumzo kulingana na jamii husika. Kanuni zilizotajwa hapa ni pamoja na kunyamaza mmoja akizungumza, urefu wa mazungumzo kwa kila mzungumzaji na mahusiano ya wazungumzaji, yaani umri, hadhi ya mzungumzaji, jinsi (mwanamke au mwanamme) na muktadha wa mazungumzo yenyewe.

Aidha, Burkart amesisitiza kuwa, ufundishaji wa kuwasiliana kwa njia ya mazungumzo unasaidia watoto kukuza uwezo wa kujua lugha kwa kuelewa wapi wanaunganisha sentensi, jinsi ya kutamka maneno vizuri na maneno gani hayafai kuzungumzwa mbele za watu.

Tassoni na Karen (2000) wanazungumzia utambulisho wa misamiati mipyä kwa watoto katika kufundisha lugha ya mazungumzo. Walimu wanatakiwa kuwapa fursa watoto kusikia na kuweza kutumia misamiati mipyä katika mazungumzo yao. Mwalimu anaweza kuainisha misamiati ambayo angependa watoto wajifunze kuzungumza na kuiingiza katika mpango wake wa kazi. Ikiwa maneno anayotaka kuyafundisha atayaweka katika mpango wake wa kazi, ni rahisi kuyatumia na watoto watajifunza kuyazungumza kwa urahisi.

Wakati Burkart (keshatajwa) ameainisha maeneo ya kutilia mkazo wakati wa ufundishaji wa stadi ya mazungumzo kuwa ni pamoja na matamshi, misamiati na kanuni za kisarufi. Tassoni (keshatajwa) anadai kuwa mambo haya ni lazima yawekwe kwenye mpango wa kazi ili mwalimu ayafundishe kirahisi.

Baker (2003) anafafanua kuwa, walimu wanaweza kufundisha wanafunzi kukuza stadi ya mazungumzo kwa kutumia njia za kufundishia stadi hii kwenye mada inayofundishwa au kwa kuandaa somo la kukuza stadi hii peke yake. Mwalimu anaweza kupanga andalio la somo ambalo linahusu ukuzaji wa stadi ya mazungumzo tu. Baker (keshatajwa) ameainisha vitendo vya kufundisha stadi hii kuwa ni kufanya kazi kwa vikundi, majadiliano na njia ya kuuliza maswali. Hii itawasaidia wale ambao si wazungumzaji sana waweze kukuza stadi hii. Aidha Baker (keshatajwa) amesisitiza kuwa watoto wanapowasilisha kazi zao, mwalimu arekebishe makosa ya kimatamshi na ya kisarufi yanayofanywa na watoto kwa njia iliyio nzuri ili watoto wafurahie mazungumzo.

Nae Intihar (2006) katika kufafanua njia za kufundishia stadi ya mazungumzo, anadai kuwa, ndani ya darasa mnakuwa na watoto wenyewe uwezo na uelewa wa aina tofauti. Hivyo basi, njia zinazotumika zitoe fursa ya kuwafanya watoto wajifunze kitu kipy. Wakati wa ufundishaji, mwalimu awe karibu sana na watoto ili wasome kwa njia ya kufurahisha na bila ya hofu. Watoto wanatakiwa waielewe mada vyema hivyo basi mwalimu afundishe misamiati mipyili watoto waielewe na waweze kuitumia katika mazingira yao.

Aidha, Intihar anaendelea kudai kuwa watoto wanapenda kuiga na kujifunza mambo mapya. Kwa hiyo katika ufundishaji wake, mwalimu atumie njia ya nyimbo, mashairi, michezo na huku anatambulisha maneno mapya kwa watoto. Nyimbo zibadilike kila baada ya muda na ziwe zenye kufurahisha na zenye maneno mapya. Kwa mfano, kupitia

nyimbo na mashairi, watoto waaweza kujifunza maneno ambayo hapo mwanzo walikuwa hawayatumii.

Wakati Baker anasisitiza vitendo vya kufundisha stadi ya mazungumzo viandaliwe andalio lake la somo na kuonesha njia ambazo zitatumika kukuza stadi hii. Intihar anawahimiza walimu kutumia njia za ufundishaji wa stadi hii ambazo zitatoa fursa ya kuzungumza ili watoto wajifunze mambo mapya.

Nayo MFL (2011) imeainisha njia ambazo zinatumika katika ufundishaji wa stadi ya mazungumzo. MFL imekuja na mpango unaoitwa ‘mkakati wa watoto wote kuzungumza’ na kuainisha njia ambazo mwalimu anapaswa kuzitumia akiwa darasani ili watoto wakuze stadi ya mazungumzo na baadaye wawe wazungumzaji wazuri. Mionganini mwa njia zilizolezwa ni pamoja na kuelezea matukio, kuelezea picha kwa kutumia maono na hisia za mtoto na kusimulia hadithi.

Pamoja na njia hizo, MFL pia imeeleza kuwa kutunga sentensi kwa njia ya piramidi ni njia bora ya ukuzaji wa stadi ya mazungumzo. Mtoto huanza na sentensi yenye neno moja, hatimaye huongeza maneno mpaka sentensi ikawa ndefu sana. Kwa mfano, mtoto anaweza kutunga sentensi kama ‘anakula’, baba anakula, baba na mama wanakula chakula. MFL amesisitiza kuwa michezo inasaidia sana kukuza stadi ya mazungumzo kwani ndani yake watoto huzungumza na kufurahi huku wengine wakijifunza maneno mapya kutoka kwa wenzao. Michezo kama ‘zungumzia juu ya unachokiona’ inawafanya watoto waeleze mambo wanayoyaona ndani na nje ya mazingira ya darasa na hivyo

hujitahidi kueleza mambo mengi, na kuwapa fursa ya kuzungumza wale wasiopenda kuzungumza.

Oradee (2012) anaeleza kuwa nadharia nyingi za ufundishaji wa stadi ya mazungumzo hasa zile zinazozungumzia mbinu ya mawasiliano, zinaweza kukuzwa kwa kutumia vitendo vya kuwasiliana ambavyo vinaweza kuwa njia za kufundishia kama michezo, maigizo, majadiliano na njia ya changanya kete ambayo inatoa fursa kwa kila mtoto kuzungumza. Jambo la msingi ni mwalimu kuandaa vitendo vya kufundishia ambavyo vinatoa fursa kwa watoto kuwasiliana na waweze kuzungumza na kufundisha misamati mipya.

Oradee na Baker hawatofautiani kwa sababu wote wamejikita katika kuangalia njia za ufundishaji wa stadi ya mazungumzo ambazo zinasisitiza uzungumzaji. Wote wametaja njia ambazo zinatoa fursa kwa watoto kuzungumza.

Shrouf (2014) anafafanua njia za kufundishia stadi ya mazungumzo kuwa ni kuandaa vitendo vya ufundishaji ambavyo vitawavutia watoto. Kwa mfano, watoto wapewe uhuru wa kuzungumza wawili au kwa vikundi na mwalimu ahakikishe anarekebisha matamshi ya watoto bila ya kuingilia kati mazungumzo yao. Mwalimu anaporekebisha matamshi ya watoto ahakikishe anatumia njia iliyo bora ili watoto wasivunjike moyo. Shrouf ameainisha njia za kufundishia stadi ya mazungumzo kuwa ni majadiliano, maigizo, bungua bongo, kuelezea picha, kusimulia hadithi na nyimbo.

Nayo The National Capital Resource Centre (2015) kama walivyonukuliwa katika mtandao wa NCRLC (2014) inafafanua kuwa wanafunzi hufikiri kwamba uwezo wa kuzungumza lugha ni matokeo ya kujifunza lugha. NCLRC (keshatajwa) inaendelea kueleza kuwa, walimu makini wanatakiwa kufundisha watoto stadi ya mazungumzo kwa kutumia njia zinazohimiza uzungumzaji. Njia zilizoainishwa ni kama zifuatazo;

- a) Kutambua maandishi yaani wanafunzi waweze kuyasoma maandishi na kuyafahamu.
- b) Kuitumia lugha kwa kuizungumza kwa usahihi kwa kuzingatia sarufi ya ile lugha.
- c) Ufundishaji wa kutumia majibu ya ana kwa ana kama vile kutumia njia ya maswali na majibu, majadiliano na vitendawili.
- d) Kubadilishana mazungumzo kama vile kuwafundisha watoto maamkizi, kuomba radhi kufanya maigizo ya kununua na kuuza pamoja na mambo yote muhimu ambayo wanafunzi wanayotakiwa wayajue ndani ya jamii yao.
- e) Kusoma kwa sauti maandishi tofauti ili waweze kuizungumza lugha.
- f) Kutenda vitendo ambavyo vitawafanya wazungumze kama vile kusimulia hadithi, nyimbo, vitendawili na ngonjera.

Njia hizi zilizoainishwa na wataalamu zikitumika ipasavyo, watoto wanaweza kukuza stadi ya mazungumzo vizuri na kuwapa wepesi wa kujifunza na vitendo vyengine vyammasomo.

Arshad (2014) anaeleza kuwa ufundishaji wa stadi ya mazungumzo unahusika na kupeleka ujumbe kwa njia ya mdomo. Arshad (keshatajwa) amegundua kuwa katika

ufundishaji wa kukuza stadi ya mazungumzo, mwalimu lazima aandae vitendo vyatukosha ili watoto waweze kuzungumza. Vitendo alivyovitaja ni pamoja na majadiliano, kazi za vikundi, maigizo na hotuba fupi.

Mawazo ya Arshad na The NCRC (wameshatajwa) ni ya aina moja. Wote wanasisitiza ufundishaji wa stadi ya mazungumzo kwa kutumia vitendo vyatukosha kama majadiliano na maigizo.

Beck (2014) anabainisha misingi ya ufundishaji stadi ya mazungumzo na kueleza kuwa mwalimu anapofundisha, anatakiwa alenge kwenye uzungumzaji wa ufasaha na kuzungumza bila ya kusitasita lakini kwa kutumia lengo alilokusudia kufundisha. Beck (keshatajwa) amehimiza kutumia njia ya kuwapa motisha watoto wakati wa ufundishaji wa stadi hii ili waweze kufurahia lugha yao. Jambo lingine lililohimizwa hapa ni mwalimu kufanya mazungumzo kuwa ni jambo la kawaida ndani ya darasa, hivyo anatakiwa atoe fursa ya kuwasiliana kwa kuanzisha mada ambayo inahimiza uzungumzaji, kuuliza maswali na kubadilishana mawazo mionganoni mwa wanafunzi. Beck (keshatajwa) pia amezungumzia suala la kutoa mrejesho kwa watoto pamoja na kusahihisha makosa ya kimatamshi kwa wakati unaotakiwa.

Kwa maoni ya wataalamu hawa, mwalimu anatakiwa awe mbunifu kwa kuanda vitendo vyatukosha vinavyohimiza na kutoa fursa kwa watoto kuzungumza na hatimaye kukuza lugha yao. Mwalimu pia anatakiwa kusahihisha makosa ya kimatamshi kwa watoto ili atakaporudia kuzungumza, aweze kusahihisha yale makosa.

Katika kujadili suala la ufundishaji wa stadi ya mazungumzo, Kayi (2006:25) anadai kuwa, mambo ya kuzingatia wakati wa kufundisha stadi hii kwa watoto ni pamoja na:

- a) Mwalimu ahakikishe matamshi sahihi ya watoto wakati wa ufundishaji ili waige maneno yaliyo sahihi.
- b) Mwalimu atumie maneno na sentensi huku akiweka mkazo, shada na kiimbo, kupanda na kushuka kwa sauti pale ambapo panastahiki.
- c) Uchaguzi wa maneno uwe sahihi na ufuate mila na desturi za pahali husika. Pia mazungumzo yalingane na hadhira husika na mada inayozungumzwa.
- d) Kupanga fikra na kuzzungumza kwa mantiki.
- e) Mazungumzo yawe na maana hasa kwa watoto.
- f) Kuzungumza kwa haraka na kwa kujiamini.

2.3 Zana za Kufundishia Stadi ya Mazungumzo Zinazotumiwa na Walimu.

Neno zana lina maana nyingi. Maana ya neno hili hupatikana kutokana na matumizi na madhumuni ya anaelitumia. Walimu wengi kutokana na kazi yao ya kufundisha wamejenga dhana ya zana kuwa na maana ya chati, picha, vitabu, ramani n.k. Zana hizi hutumika katika kukuza stadi ya mazungumzo na watoto hujifunza maneno mapya kuitia zana. (Wizara ya elimu na utamaduni; 1996). Tukichambua maana ya zana kwa kuhusisha na tendo la kufundisha mtaalamu John Vaizay kama alivyonukuliwa na Wizara ya Elimu (1996) anaeleza kuwa zana za kufundishia ni chochote kinachopangwa na kutumika katika kuinua kiwango cha elimu. Nayo Taasisi ya Elimu (2013) inafafanua kuwa zana ni vielelezo au vitu vyovoyote ambavyo mwalimu hutumia kuelezea dhana fulani, au mtoto hutumia kujifunzia dhana fulani. Kupitia dhana hizo, watoto hukuza uwezo wa kuzungumza katika matumizi ya zana.

Kutokana na usemi wa mtaalamu Vaizay, zana ni pamoja na majengo ya shule, walimu, vifaa mbalimbali. Vifaa hivi vyote pamoja na mwalimu vimepangwa na kutayarishwa kwa madhumuni ya kuinua kiwango cha elimu au tendo la ufundishaj, hivyo basi, mwanafunzi hukuza uwezo wake wa kuzungumza ikiwa mwalimu atatumia zana hizi ipasavyo.

ZMRC (2010) inaeleza kuwa katika kufundisha stadi ya mazungumzo kwa mtoto, zana za kufundishia ni kitu cha msingi sana. Mwalimu akizitumia ipasavyo katika ufundishaj wake, watoto hujifunza kuzungumza kwa urahisi. ZMRC imeendelea kueleza kuwa, kutokana na vitu ambavyo mwalimu anavitumia watoto watauliza, na kujibu maswali na kufanya majadiliano huku wakijifunza maneno mapya ambayo yatatokana na zana zinazotumiwa. Katika kufundisha stadi ya mazungumzo, wataalamu hao wamependekeza matumizi ya vitu halisi, vifani, michoro na picha ili watoto wapate kutumia milango yote ya fahamu hatimaye kukuza stadi ya mazungumzo. Stadi hii inakuzwa kwa kuuliza maswali, kujadili na kufafanua mambo ambayo yanahu zana wanazotumia, hivyo, wanafunzi wanakuza uwezo wa matumizi ya lugha ya mazungumzo.

Wizara ya Elimu (1996) inaeleza kuwa, katika ufundishaji wowote ili watoto wakuze lugha vizuri, zana za kufundishia ni kitu cha msingi sana. Watoto hukuza stadi ya mazungumzo na kuelewa somo vizuri ndani ya darasa na hata nje ya darasa.

Wizara ya Elimu inaendelea kufafanua kuwa, wakati wa ufundishaji wa stadi ya mazungumzo, zana humsaidia mtoto kutumia milango ya fahamu. Milango hii ya

fahamu haiwezi kufanya kazi ya kujifunza bila ya kuchangamshwa. Kazi ya kuchangamsha milango ya fahamu hufanywa na zana za kufundishia. Hivyo zana huchangamsha milango ya fahamu wakati wa ufundishaji wa stadi ya mazungumzo na husaidia wanalimu katika kukuza lugha ya mazungumzo kwa watoto.

Nayo Taasisi ya Elimu (2013) inatilia mkazo juu ya matumizi ya zana katika kukuza stadi ya mazungumzo kwa kudai kuwa, zana zinachangamsha milango ya fahamu, na zinakuza stadi ya kujifunza kwa mtoto kupitia mazungumzo. Taasisi ya elimu inafafanua kuwa zana zinapotumiwa na mwalimu katika kufundisha, kazi kubwa inayofanywa na mwalimu ni kuzichangamsha na kuzikuza stadi zinazotokana na milango ya fahamu ya kusikia, kuona, kugusa, kunusa na kuonja. Kwa mfano, mwalimu anapofundisha vitendawili na akawa na vitu halisi au picha za majibu ya vitendawili, watoto wataona, watagusa, wataonja na kuhusisha kitendawili na jibu lake kwa kuona zile zana ambazo mwalimu anatumia. Mwalimu atafundisha maneno mapya ambayo yametokana na lahaja au maneno ya Kiswahili sanifu.

2.4 Changamoto Zinazowakabili Walimu katika Ufundishaji wa Stadi ya

Mazungumzo

Tassoni (2002) anaeleza kuwa walimu wana hofu ya kutoa fursa kubwa ya kuzungumza kwa watoto kutokana na muda wa kufundisha ambao wanapangiwa. Tassoni (keshatajwa) anaendelea kueleza kuwa, wakati wa kupanga vitendo vyta ufundishaji, walimu hawaelewi jinsi ya kupanga muda wa kufanya mazungumzo na watoto hivyo walimu hao hujikuta wanakatisha mazungumzo na kufanya shughuli nyingine ingawaje watoto bado wanahitaji kuendeleza mazungumzo. Maoni ya Tassoni (keshatajwa)

hayatofautiani na hali halisi iliyoko katika madarasa ya elimu ya awali hapa Pemba. Walimu hawatoi fursa ya kutosha kwa watoto kuzungumza. walimu hawaipi umuhimu stadi hii kwa kuamini kuwa mazungumzo ni jambo linalotokea kila siku katika maisha hivyo wana imani watoto watazungumza tu.

Katika kutilia mkazo suala la upimaji na tathmini katika ufundishaji wa stadi ya mazungumzo, Anning (2009) amezungumzia kuwa, walimu hawapendi kujipima ili kuona ni kwa kiasi gani ufundishaji wao wa stadi ya mazungumzo umekuza uwezo wa mtoto kuzungumza lugha husika. Walimu hujiona kuwa wao ndio wenye maamuzi ya kuchagua njia na zana ambazo zitamsaidia mtoto katika kukuza stadi ya mazungumzo. Baadhi ya wakati njia na zana wanazozichagua walimu haziwasaidii watoto kwa kiasi kikubwa katika kujifunza.

2.5 Mapitio ya Kazi Tangulizi za Utafiti Kuhusu njia za Ufundishaji wa Stadi ya Mazungumzo

Katika kuchunguza namna ya ufundishaji wa stadi ya mazungumzo na kuona ni namna watoto wanakuza lugha kwa kupitia stadi hii, tafiti mbalimbali zimefanyika katika sehemu tofauti.

Abbass (2011), alifanya utafiti kwa walimu wanaofundisha Kiingereza kuhusiana na ufundishaji wa stadi ya mazungumzo katika shule ya Jacobabad Sindh nchini Pakistani. Utafiti huu ulifanyika katika shule za serikali na zinazomilikiwa na watu binafsi. Matokeo ya utafiti huu yalionesha kuwa, walimu wa shule za serikali hawakuelewa mbinu wala njia za kufundishia stadi ya mazungumzo kwa undani. Hii ni kwa sababu

walimu hawa wanatumia njia ya kusoma kwa sauti kama njia pekee muhimu ya kufundisha stadi hii. Kwa upande wa shule zinazomilikiwa na watu binafsi, walimu walitumia nyimbo, masimulizi ya hadithi, kueleza picha, majadiliano na maswali na majibu kama njia zilizo bora kufundishia stadi ya mazungumzo. Abbass (keshatajwa) amependekeza walimu wapatiwe mafunzo ambayo yatawasaidia kufundisha stadi hii.

Pamoja na kuanisha njia hizi, Abbass (keshatajwa) anaeleza kuwa, mwalimu lazima atoe fursa ya kutosha kwa mtoto kufanya vitendo mbalimbali katika mazingira yake ili aweze kuzizungumzia. Aidha, kila mtoto ashiriki katika kila kitendo ambacho mwalimu amekiandaa katika ufundishaji wake huku akibadilisha njia za kufundishia ili kila mtoto apate nafasi ya kuzungumza. Aidha, mwalimu apunguze kutoa maelezo mengi na kuwaacha watoto wazungumze huku akiuliza maswali ya wazi ambayo yataruhusu uzungumzaji. Mwalimu anaposahihisha makosa ya kimatamshi ahakikishe anatumia njia nzuri ambayo haitawavunja moyo watoto. Pia mwalimu ahakikishe kuwa vitendo kama vile nyimbo, maigizo, hadithi ambavyo anavitumia kwa ufundishaji wa stadi ya mazungumzo vinakwenda mpaka nje ya darasa. Wakati wa ufundishaji, mwalimu azunguke darasani kuhakikisha kuwa watoto wote wanazungumza. Mwalimu awasaidie watoto wale ambao watakuwa na shida ili wasiachwe nyuma na wale walio wepesi. Kwa mfano, mwalimu anaweza kuwaauliza maswali zaidi wanafunzi ambao hawapendi kuzungumza. Misamiati inayotaka kufundishwa itambulishwe kwa watoto.

Utafiti huu unahu ufundishaji wa stadi ya mazungumzo katika kisiwa cha Pemba. Hivyo, utafiti huu umeshughulikia pengo ambalo halikushughulikiwa na utafiti wa Pakistani.

Nchini Thailand, Oradee (2012) alitumia nadharia ya kukuza stadi ya mazungumzo kwa vitendo vya mawasiliano kufanya utafiti wa kuangalia ufundishaji wa stadi ya mazungumzo kwa watoto wa darasa la pili. Matokeo ya kuwa watoto wakifundishwa stadi ya mazungumzo bila kutumia njia shirikishi hawajifunzi vizuri. Lakini walimu walipofundisha kwa kutumia njia ya majadiliano, utatuzi wa tatizo na njia ya maigizo watoto walikuza stadi yao ya mazungumzo vizuri sana.

Aidha, matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa vitendo hivi mwalimu akivitumia ipasavyo katika ufundishaji wake, watoto wanakuza stadi ya mazungumzo kwa haraka.

TZ 21 (2010) ilifanya utafiti hapa Pemba kuhusiana na njia za ufundishaji wa stadi ya kusoma. Matokeo yalionyesha kuwa walimu hawatumii njia bora katika ufundishaji wa kusoma, hivyo basi wanafunzi hawashiriki vizuri katika mazoezi ya pamoja ambayo yatawafanya wazungumze.

TZ 21 (keshatajwa) ilipendekeza njia za fikiri jozisha, mgeukie jirani yako, majibu ya kadi, bana kadi na majibu ya pamoja. Aidha, **TZ21** ilieleza kuwa, mwalimu akitoa fursa kwa wanafunzi kusoma wawili katika vikundi vidogo, wanaongeza hamu ya kujifunza kusoma hivyo inamrahisishia mwalimu katika ufundishaji wa stadi hii. Njia ya kujibu pamoja huwasaidia wanafunzi wasiolelewa vyema kusoma. Mwalimu inampasa awe mbunifu wa kuteua njia ambayo itawasaidia wanafunzi waweze kusoma.

Hata hivyo, utafiti huo haukuhusu ufundishaji wa stadi ya mazungumzo katika lugha ya Kiswahili katika kisiwa cha Pemba. Aidha utafiti huo umeziba pengo hilo ambalo halikushughulikiwa na utafiti uliofanywa na **TZ21** .

2.6 Mapitio ya Kazi Tangulizi za Utafitikuhusu Zana za Kufundishia Stadi ya Mazungumzo

O'hara (2004:200) alifanya utafiti nchini Uingereza wa kuchunguza matumizi ya zana za kufundishia stadi ya mazungumzo katika darasa lenye wanafunzi wengi na wa umri kati ya miaka 3 na 5. Matokeo ya utafiti yalionesha kwamba watoto wakubwa ndio wenye fursa ya kutumia zana hizo na kuwaacha wale wadogo wakawa kimya bila ya kujua la kufanya.

Aidha matokeo ya utafiti huo yalionyesha kwamba katika darasa lenye watoto wengi na wa umri tofauti, mwalimu asipopanga darasa lake vizuri, watoto wengi hasa wadogo watakuwa hawajifunzi. Matokeo pia yalionesha kuwa mwalimu hataweza kufundisha kwa umakini misamiati ambayo amekusudia watoto waielewe hivyo wanafunzi hawatamudu vema stadi ya mazungumzo.

Hata hivyo, utafiti huo haukuhusu ufundishaji wa stadi ya mazungumzo katika lugha ya Kiswahili katika kisiwa cha Pemba. Aidha utafiti huu umeziba pengo hilo ambalo halikushughulikiwa na utafiti uliofanywa na O'hara.

Nae Tassoni (2002) alichunguza namna zana zinazotumika katika michezo ya nje zinavyokuza stadi ya mazungumzo. Utafiti huo umefanyika katika shule ya awali ya na

shule ya awali ya ABC nchini Uingereza. Matokeo ya uafiti yalionesha kuwa kutumia zana kama kamba, mipira, vikopo, firimbi na chupa watoto hujifunza misamiati kama kuruka, kudaka, kuchenza na maneno mengine mengi.

Aidha, matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa, matumizi ya zana katika ufundishaji wa stadi ya mazungumzo si lazima iwe ndani ya darasa. Tassoni (keshatajwa) anaeleza kuwa watoto wanapokuwa kwenye michezo ya nje, mwalimu anayo nafasi ya kufundisha stadi ya mazungumzo kwa kutumia zana ambazo zinatumika kwenye michezo. Kwa mfano wanafunzi na walimu wanaweza kuzungumza mambo yanayohusu hiyo michezo hivyo walimu wakachukua hiyo fursa na kufundisha watoto stadi hii ya mazungumzo kwa kutumia zana ambazo zipo kwenye michezo.

Hata hivyo, utafiti huo haukuhusu ufundishaji wa stadi ya mazungumzo katika lugha ya Kiswahili katika kisiwa cha Pemba. Ingawaje utafiti huu ulifanyika katika shule za awali, lakini shule hizi sio za kisiwani Pemba. Aidha utafiti huu umeshughulikia pengo hilo ambalo halikushughulikiwa na utafiti uliofanywa na Tassoni.

2.7 Mapitio ya Kazi Tangulizi za Utafiti kuhusu Changamoto za Ufundishaji wa Stadi ya Mazungumzo.

Wataalamu mbalimbali wa isimu wamegundua kuwa, kuna changamoto wanazokabiliana nazo walimu katika kkufundisha stadi ya mazungumzo ili wanafunzi waweze kukuza lugha.

Oseno (2010) alifanya utafiti kuhusiana tatizo la stadi ya mazungumzo kwa vijana waliomaliza darasa la nne nchini Kenya mwaka 2010. Matokeo ya utafiti huo yalionesha kuwa, wingi wa idadi ya wanafunzi kulingana na njia za ufundishaji ambazo hutumiwa na walimu, pamoja na athari za lugha ya kwanza ndio changamoto kubwa katika ukuzaji wa stadi ya mazungumzo.

Vilevile matokeo ya utafiti huo yalionesha kuwa watoto wanapotoka katika jamiilugha zilizo tofauti ufundishaji wa stadi ya mazungumzo unakuwa ni mgumu kwani watoto huwa wameathiriwa zaidi na lugha zao za kwanza.

Hata hivyo, utafiti huo haukuhusu visiwa vya Pemba. Kwa hiyo utafiti wetu huu umejaribu kushughulikia hilo pengo kwa kuchunguza ufundishaji wa stadi ya mazungumzo katika madarasa ya elimu ya awali Pemba kwa kuzingatia vipengele vya njia, zana za ufundishaji wa stadi hii na changamoto za ufundishaji wake.

2.8 Muhutasari

Sura hii ya pili imechambua kwa kina mawazo ya wataalamu kuhusiana na njia za kufundishia stadi ya mazungumzo, zana za kufundishia stadi ya mazungumzo na changamoto zinazowakabili walimu katika ufundishaji wa stadi ya mazungumzo. Tafiti mbalimbali zinazohusu ufundishaji wa stadi ya mazungumzo, zana za kufundishia pamoja na tafiti zilizofanywa kuhusu changamoto zinazowakabili walimu katika ufundishaji wa stadi hii zimejadiliwa. Hata hivyo hakuna maandiko mengi ya Tanzania yalioandika kuhusiana na stadi ya mazungumzo hasa katika ngazi ya elimu ya watoto wadogo, hivyo mapitio mengi yalijikita katika kuangalia stadi hii sehemu nyingine za

dunia. . Kwa ujumla imeonekana kuwa wataalamu wa lugha wa hapa Zanzibar hawakujikita sana katika kuchunguza ufundishaji wa stadi ya mazungumzo. Utafiti huu umezama katika kuchunguza ufundishaji wa stadi ya mazungumzo katika madarasa ya elimu ya awali hapa kisiwani Pemba katika wilaya ya Chake Chake. Utafiti umeziba pengo hilo kwa upande wa kisiwa cha Pemba.

SURA YA TATU

3.0 MBINU ZA UTAFITI

Sura hii inashughulika na mbinu mbalimbali ambazo zimetumika katika mchakato wa kufanya utafiti. Sura hii imegawanyika katika sehemu nane. Sehemu ya kwanza inajadili usanifu wa utafiti. Sehemu ya pili inajadili eneo la utafiti na sababu za kuteua eneo hilo. Sehemu ya tatu imejadili usampulishaji kwa kuangalia aina za walengwa waliotafitiwa. Sehemu ya nne imejadili jinsi mtafiti alivyopata sampuli. Sehemu ya tano imejadili mbinu mbalimbali zilizotumiwa na mtafiti katika kukusanya data. Sehemu ya sita imejadili maadili ya utafiti kwa kuangalia haki za mtafitiwa. Sehemu ya saba inaeleza kwa ufupi jinsi data zilivyochanguliwa, majadiliano na matokeo ya matokeo ya majadiliano. Sehemu ya nane inatoa muhutasari wa sura nzima.

3.1 Mkabala wa Utafiti

Mkabala wa utafiti huu katika sehemu kubwa ni wa maelezo. Usanifu wa maelezo kama ulivyofafanuliwa na Cohen (2007) ni kupanga, kutoa sababu na kuzieleza data kama zilivyoelezwa na walengwa wa utafiti. Mtafiti huzipanga kutokana na maudhui au makundi yanayofanana. Mtafiti alikuwa makini katika kueleza, kufafanua, kuhakiki, kuvumbua, kufanya majoribio, kutafsiri taarifa alizozipata kuitopia muundo huu wa utafiti. Sehemu ndogo ya utafiti imetumia takwimu kama kielelezo.

3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu unahusu ufundishaji wa stadi ya mazungumzo katika shule za awali. Utafiti umefanyika katika kisiwa cha Pemba. Kisiwa cha Pemba ni moja kati ya visiwa viundavyounda Zanzibar ambayo ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kisiwa cha Pemba kimezungukwa na Bahari ya Hindi na kiko upande wa mashariki ya Tanzania Bara. Wapemba wengi wanatokana na kabilia la Waswahili na baadhi yao wamechanganya na Waarabu wa Oman kama historia inavyosema.

Kisiwa cha Pemba kina urefu wa maili 42 na upana wake ni maili 14 na eneo lake lote ni maili 380 za mraba. (Idara ya Ardhi na Upimaji; 2014). Kisiwa hiki kina mikoa miwili tu, mkoa wa Kusini na mkoa wa Kaskazini. Kila mkoa una wilaya mbili. Utafiti huu umefanyika katika wilaya ya Chake Chake, mkoa wa Kusini.

Utafiti huu umefanyika katika sehemu mbili, uwandani na maktabani. Kwa upande wa uwandani jumla ya shule ishirini zilizoko katika wilaya ya Chake Chake, mkoa wa Kusini, Pemba zilipitiwa. Shule hizi ziliteuliwa katika majimbo manne yaliyopo katika wilaya ya Chake Chake. Kila jimbo lilipata fursa ya kuteua shule tano. Eneo hili la Chake Chake limeteuliwa kwa kuwa ndio wilaya ambayo ina shule nyingi za awali, kituo cha walimu na ofisi ya wakaguzi wa elimu. Hivyo eneo hili lilikuwa ni kiwakilishi kizuri cha maeneo mengine katika kisiwa cha Pemba.

Sababu nyingine ya kuchagua shule hizi ni kuwa hakuna utafiti wa aina ye yote amba uumefanyika katika shule hizi kuhusu ufundishaji wa stadi ya mazungumzo ya lugha ya Kiswahili.

3.3 Usampulishaji

Usampulishaji kama alivyoueleza Adam (2008) ni mbinu, mchakato au kitendo cha kutafuta walengwa wa utafiti. Nae Kothari (2004) anasema kuwa usampulishaji ni mpango wa kuchagua sampuli maalumu kutoka katika kundi kubwa.

Katika kufanya utafiti huu, walengwa walikuwa ni walimu wa shule za awali za wilaya ya Chake Chake ambao wanafundisha Kiswahili. Kila shule iliteua walimu watatu ambao wanafundisha Kiswahili. Wakaguzi wa elimu ya awali na mratibu wa kituo cha walimu waaliteuliwa kushiriki kwenye utafiti kwa sababu wanahuksika katika kukuza ufundishaji wa lugha katika shule husika. . Jedwali namba 2 linadhihirisha idadi ya walimu, idadi ya shule mtawanyiko wa shule zilizoteuliwa.

Jadwali 1 : Aina ya walengwa waliohojiwa katika utafiti

AINA YA WALENGWA	WANAWAKE	WANAUME
Mratibu wa kituo cha walimu wa shule za awali	1	0
Wakaguzi wa elimu ya awali	1	1
Walimu wa shule za awali	56	0

Chanzo : utafiti wa uwandani (2015)

3.4 Sampuli

Kutokana na idadi ndogo ya walimu katika shule za elimu ya awali, mtafiti alilazimika kuwahoji walimu wote wa shule zilizoteuliwa. Mtafiti alilazimika kuteua sampuli hiyo ambayo ndio imewakilisha walimu wa shule za awali za wilaya ya Chake Chake. Adam (2008) anaeleza kuwa, ni vigumu kwa mtafiti kushughulikia idadi kubwa ya wanajamii

wanaohusika katika utafiti hata kama anaona watafitiwa wote ni muhimu. Mtafiti hutakiwa kuchagua idadi maalumu ya wanajamii wa kushughulikia katika utafiti wake Wilaya ya Chake Chake ina jumla ya shule za awali 29. Shule zinazomilikiwa na serikali ni 15, shule zinazomilikiwa na watu binafsi ni 6 na shule zinazomilikiwa na wanajamii ni 8.

Katika uteuzi wa sampuli, vigezo vifuatavyo vilitumika; kuteuliwa walimu kutoka shule 8 za serikali, shule 6 za binafsi na shule 6 za jamii. Vigezo hivi vimezingatia uwakilishi kutoka aina zote za shule ili data zitakazopatikana ziwe za kuaminika. Kila shule iliyoteuliwa ilitoa walimu watatu wa madarasa ya elimu ya awali ili washiriki katika utafiti.

Wilaya ya Chake Chake ina wakaguzi wawili tu wa elimu ya awali na mratibu mmoja wa kituo cha walimu. Hawa ndio wasimamizi, wafuatiliaji na wafanyakaji tathmini wa ufundishaji wa stadi ya mazungumzo. Hivyo wamesaidia kutoa data ya ufundishaji wa stadi ya mazungumzo jinsi wanavyouona.

Kwa upande wa uteuzi wa washiriki, uteuzi wa sampuli rahisi ndio umetumika kutokana na idadi ndogo ya walimu hawa. Mtafiti aliteua walengwa hawa kwa kuamini kuwa alipata data ambazo zingesaidia kujibu maswali ya utafiti. Jedwali namba 1 linadhihirisha idadi ya walimu, idadi ya shule mtawanyiko wa shule zilizoteuliwa.

Jadwali 2 : Shule zilizofanyiwa utafiti (idadi ya walimu ni pamoja na walimu wakuu)

SHULE ZA SERIKALI	IDADI YA WALIMU	SHULE ZA JAMII	IDADI YA WALIMU	SHULE ZA BINAFSI	IDADI YA WALIMU
Madungu	6	Mulku	3	ABC Nursery	2
Michakaini	3	Hidayatul Atfal	2	Star	3
Machomane	7	Swafa	4	151 KJ (Jeshini)	3
Mbuzini	2	Nuur	2	Kijangwani	3
Pondeani	2	Istiqaama	2	Ibn Abbass	2
Wawi	2	Al Khalil	2	Huda	2
Wesha	2				
Al Sadiq	2				
JUMLA	26		15		15

Chanzo : utafiti wa uwandani (2015)

3.5 Mbinu za Kukusanya Data

Data kama anavyoeleza Adam (2008) ni vielelezo vinavyokubalika ambavyo vinathibitisha ukweli wa matokeo. Data za msingi (awali) kama anavyozieleza Kothari (2004) ni zile data ambazo hukusanya kwa mara ya kwanza uwandani. Data hizi zimekusanya wakati mtafiti yuko uwandani, katika shule na sehemu zilizoteuliwa.

Data hizi ndizo na zimejibu maswali ya utafiti. Data hizi zilizokuwa zimechambuliwa kwenye madaftari na simu ya mkononi zilitumika kwa ajili ya kurikodi taarifa.

Kothari (2004) anaeleza kuwa data za upili ni zile ambazo tayari zilishakusanywa na zimeshatumika na zimehifadhiwa. Data hizi pia mtarufi alizipata kuitia maandiko ya wataalamu mbalimbali pamoja na ripoti za aina tofauti. Taarifa hizi pia zilikusanywa kwa kuangalia kazi zilizopita kuhusiana na mada kwa kuangalia vitabu, majarida, na mashapisho mbalimbali katika maktaba kuu Pemba, maktaba ya chuo cha Ualimu Wete, maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na kwenye tovuti na mitandao ambayo inahusu ufundishaji wa stadi ya mazungumzo.

Katika utafiti huu mbinu mbili zilizotumika katika kukusanya data ni mahojiano na ushuhudiaji. Data nyingine zilipatikana katika tovuti.

3.5.1 Mbinu Ya Mahojiano

Hii ni mbinu ambayo mtarufi anakusanya data akiwa ana kwa ana na mtarufiwa. Mtarufi huuliza maswali na majibu huyarikodi katika daftari la kumbukumbu au kwa kutumia vifaa vya kurikodia kama vile tepu ya kurikodi au simu (Kothari 1990). Kothari anaeleza kuwa mbinu hii inahusu mchakato wa kuuliza maswali. Mtarufi anaweza kufafanua maswali ambayo hayaleweki na mtarufiwa.

Mtarufi alikwenda kuonana na walimu 56 wa shule za awali, wakaguzi wa elimu ya awali wawili na mratibu mmoja wa kituo cha walimu wa madarasa ya elimu ya awali. Mtarufi alifanya nao usaili na kurikodi taarifa zinazohusu njia za ufundishaji wa stadi ya

mazungumzo, zana zinazotumika katika ufundishaji pamoja na changamoto zinazokabili ufundishaji wa lugha ya mazungumzo.

Mtafiti alichagua mbinu hii kwa sababu ina manufaa mengi kama vile kupata fursa ya kufafanua maswali pale ambapo mtafitiwa atakuwa hakufahamu. Ikiwa mtafiti atajenga mashirikiano mazuri na watafitiwa, atapata data za uhakika.

Vilevile mbinu hii ilipoteza muda kwani mtafiti aliwafuata watafitiwa na baadhi yao asiwakute. Mtafiti ilibidi apange muda mwinigine wa kuwafuata watafitiwa.

Mbinu hii ndio iliyotumika kwa kiwango kikubwa kwa sababu ilisaidia kuhakiki na kuthibitisha matokeo ya majibu ya maswali walioulizwa walimu. Mtafitiwa alitakiwa ajibu maswali ya utafiti akiwa peke yake. Hii ilisaidia sana kupata maoni ya moja kwa moja kutoka kwa watafitiwa.

3.5.2 Mbinu ya Ushuhudiaji

Mtafiti alikusanya data kwa njia ya ushuhudiaji akiwa uwandani. Adam (2008) anaeleza kuwa ushuhudiaji ni mbinu ambayo mtafiti anakusanya taarifa kwa kushuhudia na kushiriki katika mazingira halisi. Mtafiti anatakiwa aweke kumbukumbu za taarifa ambazo anazihitaji katika daftari ama sehemu alioiweka makusudi kwa kazi hii. Matumizi ya mbinu hii ni lazima mtafitiwa awepo kwenye uwanda ili kupata taarifa kwa usahihi, ni lazima atumie viungo vya hisia iliwemo kuona kusikia, kugusa, kunusa na kuonja. Ili ushuhudiaji uwe wenye kuleta mafanikio, mtafiti atakuwa makini katika

kuandika taarifa, kuvifiki vipengele vyote anavyotaka kuvishuhudia na kuwa na muda wa kutosha.

Mtafiti alitumia mbinu hii kwa kushuhudia ufundishaji wa stadi ya mazungumzo ndani ya darasa kwa kutumia orodhahakiki. Mtafiti aliandaa orodhahakiki ambayo iliandikwa vitendo ambavyo mtafiti alitaka avishuhudie na kuitumia katika kukusanya data (angalia Kiambatisho 3). Manufaa ya mbinu hii ni kuwa mtafiti anapata ufhamu wa kina kuhusiana na mada anayoitafiti, pia huilewa vyema jamii anayoifanyia utafiti.

Pamoja na hayo, mbinu hii inaweza kuwa na mapungufu ikiwa watafitiwa watajua kuwa wanafuatiwa wanaweza kufanya mambo tofauti na uhalisia wake.

3.6 Maadili ya Utafiti

Ili kufanikisha utafiti huu, ni lazima mtafitiwa aelezwe maadili ya utafiti ili aweze kutoa taarifa za ukweli na uhakika. Aeker (2002) kama alivyonukuliwa na Adam (2008), wametaja maadili ya utafiti kuwa ni pamoja na haki ya kuwa na usiri, yaani mtafiti kutotoa siri ya mtafitiwa. Pia ameeleza haki ya mtafitiwa kuhakikishiwa usalama wake, haki ya kujua madhumuni ya utafiti, haki ya kupata matokeo ya utafiti, haki ya kujibu swalii atakalopenda kujibu na haki ya kukataa kushiriki kwenye utafiti.

Mtafiti ametambua haki zote hizi na kuzitekeleza kwa kuwaeleza watafitiwa maadili ya utafiti. Mtafiti pia aliwataka watafafitiwa kueleza kama wako tayari kushiriki katika utafiti. Kwa bahati nzuri, watafitiwa wote walikubali kushiriki katika utafiti. Tatizo lolote litakalotokea itakuwa ni juu ya mtafiti mwenyewe.

3.7 Uchambuzi wa Data, Matokeo na Majadiliano ya Matokeo

Katika utafiti huu, data zilizopatikana zilichambuliwa na kuhakikiwa kwa kina. Data zilihakikiwa na kupitiwa kwa makini kwa kupangwa katika makundi kwa mujibu wa maswali ya utafiti. Data za aina moja ziliwekwa pamoja ili kurahisisha usomaji wa maudhui yaliyokusudiwa.

Uchambuzi wa data umehusiana na malengo mahsusini ya utafiti huu na kuona ukweli ambao umepatikana kwa njia ya majadiliano na uchunguzi wa uwandani. Majadiliano ya ana kwa ana pamoja na uchunguzi wa darasani umetupatia picha halisi kuhusiana na ufundishaji wa stadi ya mazungumzo katika shule za awali za hapa Pemba. Baada ya kukusanya taarifa na kuzipanga pamoja,, uchanganuzi wa data ulifanyika kwa kuangalia takwimu ya majibu ya walimu katika matumizi ya njia mbalimbali za kufundishia pamoja na matumizi ya zana za kufundishia. Kwa upande wa ushuhudiaji wa darasani, orodhahakiki ilitumika katika kurikodi vitendo vya ufundishaji. Mahojiano ya ana kwa ana yalifanyika kwa kutumia orodha ya maswali aliyokuwa nayo mtafiti. Majibu ya aina moja yaliwekwa pamoja na kufanyiwa asilimia.

Matokeo ya taarifa yametolewa maelezo pamoja na kuchanganuliwa kwa njia ya majadweli na maelezo ili kuweka wazi matokeo yake.

Data za maelezo zilikusanywa kwa kutumia njia ya ukusanyaji data ya mahojiano. Mtafiti alipata fursa ya kufanya mahojiano na walimu, walimu wakuu, wakaguzi wa walimu elimu ya awali wa lugha ya Kiswahili na mratibu wa kituo cha walimu ili kupata maelezo ya namna ya ufundishaji wa stadi ya mazungumzo.

Aidha, mtafiti alikusanya data kwa kushuhudia ufundishaji wa stadi ya mazungumzo ndani ya darasa. Orodhahakiki ilitumika katika kurikodi taarifa. Njia hii imerahisisha kukusanya taarifa na kuzichambua kwa umakini.

3.8 Muhutasari

Sura hii imechambua mbinu za utafiti. Usanifu wa maelezo na takwimu umeelezwa na jinsi ulivytumika. Eneo la utafiti umetajwa kuwa ni wilaya ya Chake Chake, mkoa wa Kusini, Pemba. Walengwa wa utafiti wameainishwa kuwa ni walimu, wakaguzi wa elimu ya walimu na mratibu wa kituo cha walimu. Njia ya mahojiano na ushuhudiaji zimeelezwu kuwa zimetumika katika kukusanya data za utafiti. Maadili ya utafiti yameelezwu. Uchambuzi wa data, uwasilishaji na majadiliano matokeo ya yameelezwu kwa ufupi.

SURA YA NNE

4.0 UCHAMBUZI WA DATA, UWASILISHAJI NA MAJADILIANO YA MATOKEO

4.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha data zilizopatikana uwandani na maktabani. Uchambuzi wa data umefanyika kwa kutumia misingi na kanuni za kiunzi cha nadharia ya ufundishaji ya mawasiliano ya Firth (1970) na Hymes (1971).

Uchambuzi wa data ulilenga kujibu maswali ya utafiti huu katika kukamilisha malengo ya utafiti. Sura hii imegawanyika katika sehemu nne. Sehemu ya kwanza inachambua data inayohusu njia za kufundishia zinazotumiwa na walimu katika kufundisha stadi ya mazungumzo kwa watoto. Sehemu ya pili inachambua data inayohusu zana za kufundishia stadi hii ambazo walimu huzitumia. Sehemu ya tatu inachambua changamoto wanazokabiliana nazo walimu katika kukuza stadi ya mazungumzo, na sehemu ya mwisho ni hitimisho. Uchambuzi wa data umehusishwa na malengo mahsusini ya utafiti huu na kwa kujibu maswali ya utafiti.

4.2 Njia Zilizotumika katika Ufundishaji wa Stadi ya Mazungumzo

Tafiti zinaonyesha kuwa kuna mambo yanayochangia katika kushuka kwa kiwango cha ufundishaji usioridhisha madarasani kama ilivyoelezwa na Mtana, 2003. Swali mojawapo la kujiuliza ni kuwa; Je, ni njia gani zinatumika katika ufundishaji wa stadi ya mazungumzo? Hapa tunaweka wazi baadhi ya njia za kufundishia stadi ya mazungumzo katika lugha ya Kiswahili.

Matokeo ya utafiti huu kutohana na majibu ya walimu kutoka shule za serikali, wakijibu swali juu ya njia ambazo wanatumia kufundisha stadi ya mazungumzo ili wanafunzi waweze kukuza lugha yameonesha kwamba, asilimia 37.5% (21) tu ya walimu wote waliohojiwa ndio wanatumia njia shirikishi.

Baadhi ya njia shirikishi walizotaja ni majadiliano, maswali na majibu na hadithi. Njia hizi zimetajwa kuwa zinasaidia walimu kufundisha misamiati mipyä pamoja na kuhimiza matumizi ya sentensi kwa usahihi. Matokeo yanaashiria kwamba, idadi na asilimia ya walimu wanaotumia njia shirikishi kufundisha stadi hii iko chini ya wastani (37.5%), hivyo wanafunzi wanaofundishwa kikamilifu stadi hii ni wachache sana.

Matokeo ya walimu walioshuhudiwa darasani wakifundisha pia yameonesha kwamba, asilimia 42.8% (24) tu ndio wanafundisha lugha ya mazungumzo kwa njia shirikishi zilizotajwa hapo juu pamoja na nyimbo, ziara, ngonjera, vitendawili na matumizi ya vikaragosi.

Matokeo ya uchambuzi wa data yameonyesha kwamba asilimia 25 % (14) ya walimu wa shule za jamii na watu binafsi wanafundisha watoto stadi ya mazungumzo kwa njia ya kuwasemesha, majadiliano, nyimbo, hadithi, maswali na majibu na vitendawili. Walimu hawa, hasa ambao hawakupata mafunzo ya ualimu vyuoni, walionesha kutofahamu njia shirikishi katika ufundishaji wa stadi hii.

Matokeo ya utafiti huu kuhusu njia za kufundishia stadi hii kwa jumla yameonesha kuwa 57% (32) hawafundishi stadi ya mazungumzo kwa njia shirikishi. Matokeo haya

yanaashiria kuwa wanafunzi walio wengi hawajifunzi vema stadi ya mazungumzo. Hii ni kwa sababu njia shirikishi ndio huaminika kuwasaidia watoto kukuza stadi ya mazungumzo kama alivyositisiza Mtana (2003) kwamba, mwalimu akitumia njia shirikishi katika ufundishaji wake watoto watakuza stadi ya mazungumzo.

Kwa sababu hii tunadiriki kusema kuwa, moja ya sababu zinachochangia wanafunzi wengi kushindwa kujifunza vema stadi ya mazungumzo ni kushindwa kwa walimu kuwafundisha watoto stadi ya mazungumzo kikamilifu kwa njia shirikishi.

Mtafiti alishuhudia walimu wakieleza mambo mengi na kuyarudia tena na tena ili watoto wayakumbuke. Walimu wanasaahau kuwashirikisha watoto ili waweze kutumia maneno hayo, kuunda sentensi na hatimae waweze kukuza stadi ya mazungumzo. Njia za kufundishia stadi ya mazungumzo ambazo zimeainishwa na walimu na pia kushuhudiwa na mtafiti zinawasilishwa.

Data hizi zilikusanywa kwa njia ya kufanya mahojiano na watafitiwa pamoja na ushuhudiaji. Maswali ya mahojiano pamoja na orodhahakiki ziliandaliwa mapema ili kurahisisha zoezi. Data zilipangwa na kuhakikiwa kuona ni wahojiwa wangapi walitoa majibu ya aina moja kulingana na hoja iliyoulizwa au kushuhudiwa na kuweka asilimia. Wahojiwa waliangaliwa ikiwa wanatoka katika shule za serikali, za jamii au zinazomilikiwa na watu binafsi ili kupata picha halisi. Mwisho wa zoezi mtafiti alifanya majumuisho.

4.2.1 Majadiliano kama Njia ya Kufundishia Stadi ya Mazungumzo.

Mtafiti alifanya mahojiano na walimu 56 katika shule 20 kama wanatumia njia ya mahojiano katika kufundisha stadi ya mazungumzo. Aidha, mtafiti alishuhudia ufundishaji wa stadi hii ukifanywa na walimu. Matokeo yalionesha kwamba asilimia 33.6% (19) kati ya walimu 56 tu ndio wanaofundisha watoto stadi hii kwa kutumia njia ya majadiliano.

Matokeo ya utafiti ya utafiti huu yanaashiria kuwa, walimu hawaamini kuwa watoto wanaweza kutumia lugha yao kutoa mchango wao kuhusiana na mada husika kutokana na umri wao. Ushuhudiaji huu ulionesha kwamba baadhi ya walimu 24 (42.8%) wakati mwingine walishindwa kuongoza vizuri majadiliano, hivyo kutoa maelezo mengi ambayo yaliwanyima watoto fursa ya kuzungumza na kukuza lugha yao. Hali hii iliwasababishia watoto wakimya kutozungumza kabisa na kushindwa kutumia misamiati mipy. Mara chache mno walimu walitoa fursa kwa watoto kushiriki kutafuta maana ya maneno mapya kwa kuyaeleza wenyewe. Katika njia ya majadiliano, mawasiliano hutoka pande zote, yaani kutoka kwa mwalimu na watoto (Mtana 2003). Njia hii humwezesha mwalimu na watoto kuwasiliana kwa urahisi. Mwalimu hufanya kazi ya kuongoza majadiliano ili hali watoto ndio wazungumzaji wakuu. Kwa njia hii, watoto hupata nafasi ya kujadili kuhusu maana walizo nazo na wanapofikia muafaka, kila mmoja anatarajiwa kuwa amepata maana ya nyongeza kutoka ile aliyokuwa nayo awali kuhusu mada husika. Hapo mtoto anakuwa amejifunza jambo la ziada na kukuza stadi yake ya mazungumzo. Jukumu la mwalimu katika ufundishaji wake ni kusaidia kuweka sawa misamiati na miundo ya sentensi iliyokosewa pamoja na kurekebisha matamshi.

Mtana anaeleza kuwa njia ya majadiliano ikitumiwa ipasavyo huweza:

- a) Kukuza uhusiano kati ya wahusika kwa kuendeleza mazungumzo.
- b) Kuwafanya wahusika wafurahie ufundishwaji wa lugha yao na walipende somo.
- c) Kukuza stadi ya mawasiliano kwa njia ya mazungumzo.
- d) Kujenga uwezo wa wahusika wa kujiamini na kuvumiliana wakati wa kuzungumza.
- e) Kumpunguzia mwalimu jukumu la kueleza kila kitu kwa wanafunzi wakati wa ufundishaji.

Majadiliano humwezesha mwalimu kuelewa kiwango cha msamiati wa wanafunzi wake na uwezo wao wa kuzungumza. Kuelewa huku huweza kumwezesha mwalimu kuwasaidia watoto kukuza na kupanua kiwango chao cha lugha wakati anapofundisha. Aidha,, mtafiti ameshuhudia walimu wote 24 (42.8) wana mapungufu katika stadi ya kuunda maswali ya mjadala. Katika kutazama jinsi mijadala ilivyofanyika darasani, katika shule ya Madungu, mtafiti alishuhudia watoto wakipewa picha ili kujadili. Wanafunzi walipojibu kuwa wameona bahari, mashua, watu. Mwalimu hakutoa fursa ya kuendeleza mazungumzo ambayo yangetokana na picha ile. Picha ilikuwa imechorwa vizuri, mandhari ya kuvutia na rangi tofauti.

Wataalamu (ZMRC, 2010; Taasisi ya Elimu, 2003) wanapendekeza kuwa, katika ufundishaji wa stadi ya mazungumzo, walimu watumie zana mbalimbali kama vile vitu halisi, picha na michoro ili wachochee wanafunzi kuongea na kujadili hoja mbalimbali kutokana na vitu halisi, picha na vitendo mbalimbali darasani. Hizi zana na vitendo mbalimbali huwachochea watoto kuongea, na hivyo huwawezesha kufanya mazoezi mengi ya stadi ya kuzungumza.

Katika shule ya binafsi ya Star, mtafiti alishuhudia wanafunzi wengi ndani ya chumba kimoja wakifundishwa na mwalimu mmoja. Wanafunzi hawakuweza kuunda vikundi vizuri vyta majadiliano kutokana na wingi wao ndani ya darasa. Mwalimu aliwataka wajadiliane juu ya Maulidi ya Mtume Muhammad yalivyosomwa kwani ilikuwa ni kipindi cha Maulidi. Baadhi ya watoto hao hawakupata fursa ya kuzungumza. Watoto 5 tu kati ya watoto 32 ndio walitoa mchango wao. Waliobaki walikuwa wanajifanyia shughuli zao zingine pamoja na kusukumana wakigombea nafasi ya kukaa vizuri. Hivyo watoto hawakuweza kufanya mazoezi ya misamiati mipya ambayo waliyasikia kutoka kwa walimu wao na kwenye jamii. Takriban katika shule zote hali ilikuwa ni hiyo.

Wataalamu wengi (Baker, 2003; Intihar, 2006; Kayi, 2006) wamependekeza njia ya majadiliano itumike katika ufundishaji wa wanafunzi stadi ya mazungumzo ili waweze kukuza uwezo wao wa lugha. Katika hali halisi ya madarasani, njia ya majadiliano haitumiki kama ilivyoshauriwa na wataalamu. Hivyo basi, watoto wanashindwa kupata maarifa ya kutosha ya stadi ya mazungumzo.

4.2.2 Njia ya Maswali na Majibu katika Kufundishia Stadi ya Mazungumzo

Mtafiti aliwahoji walimu wote 56 katika shule 20 kama wanafundisha wanafunzi stadi ya mazungumzo kwa njia maswali na majibu. Matokeo ya utafiti huu kuitia majibu ya walimu yalionesha kwamba asilimia 100% (56) ya walimu hao wanafundisha watoto stadi hiyo kwa njia ya maswali na majibu.

Aidha matokeo ya utafiti huu yanaonesha kwamba asilimia 100% ya walimu walioshuhudiwa wakifundisha darasani walitumia njia ya maswali na majibu katika ufundishaji wa stadi ya mazungumzo.

Matokeo ya utafiti yameonyesha kuwa asilimia 100% ya walimu walikubali kuwa wakitumia njia hii, wanafunzi wanamudu kujieleza vyema kwa mazungumzo kuliko kwa maandishi. Matokeo haya pia yalionesha kuwa, asilimia 68% (38) ya walimu walidai wanafunzi wengi humudu kujieleza kwa mazungumzo ikiwa mwalimu atawauliza wanafunzi maswali kutokana na picha, michoro na vitu halisi vitakapotumiwa na walimu watakapofundisha.

Kinyume chake, matokeo ya data yameonesha kuwa asilimia 50% (28) ya walimu waliotazamwa darasani hawakutumia njia hii ipasavyo, hivyo walisababisha wanafunzi washindwe kujieleza kwa kuzungumza. Walimu ndio walitawala mazungumzo darasani hivyo kukwamisha kukuza uwezo wao wa kujieleza kwa mazungumzo.

Katika kutazama ufundishaji ndani ya darasa, mtafiti ameshuhudia kuwa walimu wote 56 walishindwa kuyaweka wazi maswali yao na watoto wakaweza kuzungumza kwa urefu. Takriban walimu wote 56 sawa na asilimia 100% wa shule za serikali (walimu 26), za binafsi (walimu 15) na za jamii (walimu 15) hawakuweza kuuliza maswali ya wazi ya kuwafikirisha wanafunzi ili wayajibu ipasavyo.

Maswali ya wazi kama yalivyojadiliwa na Mtana (2003) ni yale yanayotoa fursa ya kuwa na jibu zaidi ya moja. Mwalimu anapoona swali halijibiwi anashindwa namna ya

kuliweka sawa ili watoto waweze kuzungumza, hivyo huamua kulijibu mwenyewe na watoto ama wakisikiliza tu, au wakirudia alichosema mwalimu bila kuongeza chochote.

Katika shule ya Mulku ambayo ni ya jamii, mwalimu aliwatoa watoto nje na kuwaambia waangalie mazingira yaliyowazunguka, wayachunguze na baadaye warudi darasani na kuzungumzia walichokiona. Watoto walitoka nje kwa furaha na kuchunguza mazingira yao. Waliporudi darasani mwalimu aliwataka waeleze vitu walivyoviona huko nje. Matokeo ya zoezi hilo yalionesha kuwa asilimia 51% (12) ya watoto wote 25 ndio walijibu neno moja moja kama vile, ‘*majani, miti, wadudu, nyumba.....*’ Mwalimu hakuwasitisiza watoto kujibu kwa kutumia sentensi kamili. Mwisho, mwalimu aliwataka wachore hivyo vitu. Baada ya kuchora hakutoa fursa kwa watoto kuelezea picha zao wakati kwenye andalio la somo aliandika kuwa atafanya kitendo hicho

Mtafiti pia alishuhudia kuwa walimu 20 (35.7%) hawaoneshi umuhimu wa kuwahimiza watoto kuuliza maswali. Walimu wanadhani kuwa watoto hawana maswali ya kumuuliza mwalimu kwani wao ni wadogo na ni watu wa kupokea kutoka kwa mwalimu, hivyo kwa kiasi fulani wanarudisha nyuma ukuzaji wa stadi ya mazungumzo ya watoto.

Kwa upande mwingine, mtafiti alishuhudia kuwa walimu hawatoi muda wa kutosha kwa watoto kujibu maswali. Mwalimu alipouliza swali alitaka wanafunzi wajibu kwa haraka. Mwalimu alisahau kuwa watoto wadogo walihitaji muda wa kufikiri kabla ya kujibu swali. Hivyo watoto wachache walio na uwezo mzuri ndio waliopata fursa ya kuzungumza. Mwalimu alichagua hao hao kujibu maswali na kuwaacha wale

wasiokuwa wazungumzaji wakiwa wametulia wakisikiliza tu au wakijifanyia shughuli zao zisizohusiana na somo lile. Hali hii inaashiria kuwa walimu walio wengi hawana ujuzi wa kutosha wa kufundisha stadi hii ya mazungumzo hivyo kuwakosesha watoto fursa ya kukuza stadi ya mazungumzo ipasavyo.

(Abbass: 2011) amethibitisha kuwa njia ya maswali na majibu ni moja kati ya njia muhimu ya kufundishia ambayo huwapa wanafunzi fursa ya kukuza uwezo wao wa kujieleza kwa mazungumzo. Aidha, Abbass anasisitiza kuwa njia hii ni bora kuliko njia nyingine kwa sababu watoto hukuza ufahamu wao kupitia mazungumzo. Ili kukuza stadi ya mazungumzo, mwalimu aulize maswali na wanafunzi wajibu, lakini pia mwalimu atoe fursa ya kuulizwa maswali na anatakiwa ayajibu kwa ukamilifu. Wanafunzi wapatiwe nafasi ya kutosha ya kuuliza au kujibu maswali bila ya kuwakemea wala kuyapuuza maswali yao. Uhusiano wa namna hii ukiimarishwa darasani, utawawezesha wanafunzi kujenga maana ya wanachofundishwa na pia wataweza kujifunza misamiati mipyä kila siku, na si kujifunza tu bali pia wataweza kutumia misamiati hiyo.

Kutokana na matokeo ya data pamoja na hoja za hapo juu tunadiriki kusema kuwa, kushindwa kwa watoto wa Chake Chake kumudu vema stadi ya mazungumzo, kunatokana na baaadhi ya walimu kutotumia njia ya maswali na majibu katika kufundisha stadi hii kikamilifu. Baadhi ya walimu (asilimia 40%) wanashindwa kutumia njia hii kwa sababu hawana ujuzi wa kutosha wa njia ya kufundishia stadi hii kwa kuwa hawakufunzwa vya kutosha vyuoni.

4.2.3 Njia ya Hadithi / Masimulizi Katika Kufundisha Stadi ya Mazungumzo

Mtafiti alifanya mahojiano na walimu kutaka kujua kama wanatumia njia ya hadithi na masimulizi kufundishia watoto stadi ya mazungumzo. Matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha kuwa asilimia 96% (54) ya walimu waliohojiwa walifundisha stadi hiyo kwa njia ya hadithi na masimulizi.

Kwa upande mwingine asilimia 21% (12) ya walimu walishuhudiwa darasani wakifundisha watoto stadi hii bila ufanisi kwa njia ya hadithi. Aidha, asilimia 96% (54) ya walimu hao walikubali kuwa kufundisha watoto kwa njia ya hadithi kunawasaidia kukuza stadi ya mazungumzo. Matokeo hayo pia yamedhihirisha kuwa asilimia 48% (27) ya walimu wote waliohojiwa walikubali kuwa watoto wanaweza kujieleza vema wakifundishwa stadi ya mazungumzo kwa njia ya hadithi na kwa kutumia zana kama vile picha, michoro na vitu halisi.

Walimu walipotazamwa darasani, matokeo yalionyesha kuwa asilimia 21% (12) ya walimu hawaitumii njia hii ipasavyo hivyo wanasababisha wanafunzi wasiweze kujieleza kwa kuzungumza.

Mwalimu wa shule ya Michakaini alisahau kufafanua maana ya maneno. Katika shule hiyo, mwalimu alitumia maneno ya lahaja ya Kipemba na shule ni ya mjini bila ya kufafanua maana ya maneno. Maneno yaliyotumika ni:

Kipemba
Gogwa
Ntunke
Matonyo

Kiswahili sanifu
hasira
mwanamke
matone

Geleka	potea
Kivuru	nyumba ndogo ya udongo

Mtafiti alipomuuliza mwalimu kama wanafunzi walielewa maana ya maneno haya, mwalimu alijibu kuwa hana hakika kama wanafunzi wote wameyaelewa. Aidha, mtafiti alishuhudia mwalimu akiwa darasani hakuwa na ustadi kutosha ya kutoa hadithi kwa watoto. Mwalimu alishindwa kuuliza maswali au kuwashimiza watoto kubuni matukio yatakayotokea baadayeambayo yanewasaidia kuweza kutumia lugha ya mazungumzo. Walimu waliposimulia hadithi, maswali wanayouliza ni fungo kwani ni yale yaliyohitaji jibu la “ndio” au “hapana”. Mfano; “Mnamjua sungura?” “Mmesikia?” “Mmefahamu?”. Majibu yake yalikuwa, “Ndio”. Majibu ya namna hii hayakuzi stadi ya kuzungumza. Walimu wote 56 sawa na asilimia 100 waliohojiwa walitaja hadithi kuwa ni njia nzuri ya kufundishia stadi ya mazungumzo kwani wanafunzi hujifunza maneno mapya.

Mtafiti alishuhudia katika shule ya Al Khalil ambayo ni ya binafsi, mwalimu akisimulia hadithi kwa haraka mno bila lafudhi nzuri kiasi ambacho watoto walishindwa kufuatilia matukio ya hadithi. Mwalimu alipouliza wanafunzi maswali yatokanayo na hadithi, watoto walishindwa kujibu. Wakati wa mahojiano na mtafiti mwalimu huyu alijibu kuwa ana miezi sita tu ya kazi ya kufundisha somo la Kiswahili na wala hajawahi kupata mafunzo ya aina yoyote yanayohusu ufundishaji wa stadi ya mazungumzo. Hali hii iliwasababisha wanafunzi washindwe kujieleza.

Aidha, mtafiti alishuhudia walimu 2 katika shule za jamii ambazo zinapewa mafunzo na ‘Mpango wa elimu ya awali kwa watoto’ wakitumia zana katika kusimulia hadithi. Shule kama Mulku na Hidayatul Atfal, walimu walikuwa na kadi zenyenye michoro iliyo onesha matukio yaliyo ndani ya hadithi. Wakati wa kuuliza maswali yanayohusiana na matukio ya hadithi, watoto walijibu kwa ufupi na walimu hawakuwahamasisha watoto wafafanue majibu yao. Mwalimu angeliweza kuwaauliza maswali ya wazi ili wanafunzi wapate fursa zaidi ya kujieleza.

Kwa upande mwingine, mtafiti alipowahoji walimu, walieleza kuwa wanatambua umuhimu wa kutumia njia ya hadithi katika kukuza stadi ya mazungumzo. Asilimia 30% (18) ya walimu 56 walieleza kuwa hadithi ni kitu wanachokifurahia watoto, wanapenda kusimulia na kusimuliwa hadithi. Hivyo basi, ni vizuri walimu waitumie njia hii mara kwa mara ili watoto wakuze uzungumzaji wao. Kinyume chake, takriban walimu wote (asilimia 100) hawana stadi za kutosha za kusimulia hadithi na matokeo yake walishindwa kutumia kwa ufanisi njia hii na hivyo kukwamisha uwezo wa kujieleza kwa wanafunzi.

Taasisi ya Elimu (2003) inaeleza kuwa njia ya hadithi na masimulizi husaidia kukuza uwezo wa kumudu lugha ya mazungumzo kwa kuwa zina uhusiano wa maisha ya watoto, hivyo hupenda kusimulia na pia kusikiza hadithi. Taasisi ya Elimu pia inasisitiza kuwa msamiati wa lugha ambao mwalimu anatumia wakati wa kusimulia hadithi ulingane na kiwango cha wanafunzi cha kujifunza lugha. Sentensi zinazotumika kwenye hadithi ziwe fupi na maneno yawe rahisi kueleweka na watoto.

Kutokana na matokeo ya data pamoja na hoja za hapo juu tunadiriki kusema kuwa kushindwa kwa watoto wa hapa Chake Chake kumudu vema stadi ya mazungumzo, kunatokana na baaadhi ya walimu kutotumia vyema njia ya hadithi katika kufundisha stadi hii kikamilifu. Baadhi ya walimu wanashindwa kutumia njia hii kwa sababu hawana ujuzi wa kutosha.

4.2.4 Njia ya Maigizo Katika Kufundishia Stadi ya Mazungumzo.

Mtafiti alitumia mbinu ya ushuhudiaji kutazama walimu wakifundisha stadi ya mazungumzo darasani kwa njia ya maigizo. Matokeo ya utafiti yalionesha kwamba asilimia 1.7% ya walimu ndio walitumia njia ya maigizo kufundisha stadi ya mazungumzo.

Kwa upande mwingine walimu walipohojiwa na mtafiti, matokeo yalionesha kwamba asilimia 9% (5) tu ya walimu 56 ndio wanafundisha watoto stadi ya mazungumzo kwa njia ya maigizo. Matokeo ya mahojiano vilevile yalionesha kuwa maigizo hufanyika mara chache hasa wakati wa sherehe za shule za siku ya wazazi, hivyo si watoto wote wanapata fursa ya kuzungumza kupitia maigizo. Watoto wachache tu ndio wana uwezo mzuri wa kuzungumza. Watoto wengine hubaki kuwa wasikilizaji tu. Baada ya maigizo huwa hakuna fursa ya majadiliano. Inapotokea hiyo fursa, watoto wachache tu walio wasemaji sana ndio hupata fursa ya kushiriki kwenye majadiliano. Hivyo njia hii hukuza stadi ya mazungumzo kwa baadhi ya watoto tu. Katika kutilia mkazo umuhimu wa kutumia njia ya maigizo, mwalimu wa shule ya Machomane alieleza kuwa,

*“Maigizo ni njia nzuri sana ya kuwafanya watoto wakuze
stadi ya mazungumzo, lakini kuandaa maigizo na kuwatayarisha*

watoto ni kazi kubwa. Muda unapotea sana. Hivyo tunaandaa maigizo tunapokuwa na shughuli maalumu, labda sherehe za serikali na siku ya wazazi.”

Arshad (2014) anaeleza kuwa maigizo hutumika kama njia ya kufundisha ambayo inakuza stadi ya mazungumzo. Ni njia inayomsaidia mtoto kujenga mwelekeo wa watu na vitu fulani kwa njia ya kuzungumza. Katika michezo ya kuigiza, watoto huigiza matendo ya watu wengine kama wanavyoyaona au wanavyoyasikia, hivyo basi, kunakuwa na fursa ya ufundishaji wa lugha. Maigizo yanaweza kutokana na hadithi walizosimuliwa au matukio yanayotokea ndani ya jamii. Ili maigizo yaweze kuleta ufanisi katika kukuza stadi ya mazungumzo kwa wanafunzi, mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wanaigiza vitendo vya watu wanaoigwa kikamilifu iwezekanavyo. Kila mwanafunzi apewe uhusika wake huku ufundishaji wa maneno mapya, ufafanuaji wa maneno magumu pamoja na uzungumzaji wa ufasaha ukielezewa na mwalimu.

Kutokana na matokeo hayo pamoja na hoja za walimu, sababu mojawapo ya kushindwa kwa wanafunzi wa Chake Chake kumudu vema stadi ya mazungumzo ni walimu kutotumia njia ya maigizo mara kwa mara. Aidha, walimu wengi hawana ujuzi wa kutosha wa kuandaa maigizo na kuyatumia kama njia ya kufundishia lugha ya mazungumzo, ingawaje miutasari ya elimu ya awali imewaeleza walimu kufundisha stadi ya mazungumzo kwa njia maigizo.

4.2.5 Michezo na Nyimbo kama Njia ya Kufundishia Stadi ya Mazungumzo.

Mtafiti alitumia mbinu ya ushuhudiaji kwa kuwatazama walimu wakifundisha stadi ya mazungumzo kwa njia ya michezo na nyimbo. Matokeo ya utafiti kwa njia hii yalionesha kwamba asilimia 42% (24) ya walimu 60 ndio walitumia njia ya michezo na nyimbo kufundisha stadi ya mazungumzo.

Kwa upande mwengine walimu walipohojiwa, matokeo yalionesha kwamba asilimia 100% (56) ya walimu wanafundisha watoto stadi ya mazungumzo kwa njia ya michezo na nyimbo. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa, asilimia 100% ya walimu wanatumia njia ya michezo na nyimbo lakini hawaitumii ipasavyo kama ilivyopendekezwa na wataalamu.

Kwa mfano, katika skuli ya Pondeani, mwalimu alishuhudiwa akitumia nyimbo katika kufundisha irabu kwa kuimba pamoja na watoto;

*“a e i o u
 hizi ni herufi tano
 muhimu ziso mfano
 zinachanganya maneno”.*

Mwalimu hakufafanua maana ya maneno **herufi**, na **zinachanganya**. Mtafiti alimuuliza mwalimu kama wanafunzi wanaelewa maana ya maneno hayo, nae alijibu kwamba huo ni wimbo tu.

Mtafiti alishuhudia wanafunzi wa skuli ya Michakaini wakiimba na kucheza nyimbo walipokuwa wapo kwenye michezo ya nje. Michezo hii hutoa fursa nzuri kwa watoto kukuza stadi zao za mazungumzo na lugha kwa jumla.

Kwa mfano; mtafiti alishuhudia watoto wakicheza na kuimba wimbo wa seremala.

*“Seremala nipasulie mbao
Walia kweche msumeno
Wengine na baskeli zao
Wala hawataki maneno”*

Mwalimu hakufafanua maana ya misamiati kama seremala na msumeno. Mtafiti alimuuliza mwalimu kama watoto wanaelewa maana ya seremala na msumeno. Mwalimu alijibu kuwa hana hakika kama watoto wanaelewa maana ya maneno hayo.

Baker (2003) na Kayi (2006) wanaeleza kuwa njia ya michezo na nyimbo zikitumika katika ufundishaji wa stadi ya mazungumzo, watoto huweza kujifunza maneno mapya na hatimaye huyatumia katika maisha yao ya kila siku. Katika kuiangalia njia hii inavyotumika darasani, mtafiti ameshuhudia kuwa walimu hutumia njia hii sio kwenye masomo ya lugha ya Kiswahili katika kufundisha stadi ya mazungumzo tu, bali pia hutumika kwenye masomo mengine kama hisabati, sayansi, mazingira, dini na michezo.

ZMRC (2000) inaeleza kuwa baadhi ya watoto wanapokuja kuanza shule za awali, wanakuwa hawajaweza kuzungumza vizuri. Watoto hawa wanakuwa bado hawajaweza kutamka baadhi ya maneno. Hii husababishwa na mazingira wanayoishi ambayo yanawafanya wasijifunze kuzungumza vizuri. Mtafiti ameelezwa na walimu kuwa, kupitia nyimbo wanazofundishwa shulenii, watoto hawa huweza kuzungumza kwa wepesi zaidi na uzungumzaji wa kusitasita pia unapungua. Hoja ya mtaalamu huyu inaungwa mkono na mwalimu wa shule ya Madungu. Wakati wa mahojiano na mtafiti, mwalimu alieleza;

“Baadhi ya watoto wanapoletwa hapa shule huwa hawawezi kuzungumza vizuri. Wanapokaa kwa muda mchache tu Kwa vile tunawafundisha nyimbo za kuvutia Na wanaziimba, basi mara moja watoto hawa wanaweza kuzungumza”.

Kutokana na matokeo ya data na hoja za hapo juu, tunaweza kusema kuwa njia ya michezo na nyimbo hutumiwa na walimu wote (asilimia 100) katika ufundishaji. Hata hivyo njia hii inawasaidia watoto kukuza stadi ya mazungumzo kwa kiwango kidogo sana kwa sababu ingawa walimu walipohojiwa walidai kuwa wanatumia njia hii kufundisha stadi ya mazungumzo, ushahidi kutokana na ushuhudiaji umeonesha kuwa asilimia 42% (24) ya walimu ndio walitumia njia ya michezo na nyimbo, hivyo walimu wengi kutoitumia njia hii ipasavyo katika ufundishaji wa lugha ya mazungumzo.

4.2.6 Njia ya Ziara na Uchunguzi katika Kufundisha Stadi ya Mazungumzo

Mtafiti alitumia mbinu ya ushuhudiaji kwa kuwatazama walimu wakifundisha stadi ya mazungumzo kwa njia ya ziara na uchunguzi. Matokeo ya utafiti kwa njia hii yalionesha kwamba asilimia 1.7% (1) ya walimu 56 ndio walitumia njia ya ziara na uchunguzi kufundisha stadi ya mazungumzo.

Kwa upande mwingine walimu walipohojiwa, matokeo yalionesha kwamba asilimia 9% (5) ya walimu 60 walifundisha watoto stadi ya mazungumzo kwa njia ya ziara na uchunguzi.

Tukiangalia mfano katika somo la Kiswahili mada ya “***kuzungumzia mazingira yaliyozunguka shule***”, katika skuli ya Madungu, mtafiti alishuhudia mwalimu na

wanafunzi wakichunguza vitu vinavyowazunguka katika maeneo ya jirani. Baadhi ya maswali yalioulizwa na mwalimu na kujibiwa na wanafunzi yalikuwa:

Mwalimu: mmeona nini?
Wanafunzi: wadudu, nyumba, baskeli.....
(Kila mtoto alijibu alichoona)
Mwalimu: na nini tena?
Wanafunzi: panzi, zenengo, nzi, watu
Mwalimu: haya basi imetosha...
Wanafunzi: gari pia...
Mwalimu : haya, kila mtu achore alichokiona.

Changamoto kubwa iliyokuwepo ni kuwa mwalimu alishindwa kuendeleza yale maswali ili wanafunzi watumie lugha kwa umahiri katika mazungumzo. Mwalimu hakuwa na stadi ya kuuliza maswali ya wazi ambayo yanatoa mwanya wa kujibu zaidi na zaidi na hatimae wanafunzi kujenga moyo wa kujiamini katika kuzungumza na kutumia lugha ipasavyo.

Mwalimu alikuwa na fursa ya kuuliza maswali mengi zaidi ikiwemo rangi za vitu walivyoona, na matumizi ya vitu hivyo. Wanafunzi waliota jibu kwa kutaja wadudu wa aina mbalimbali. Mwalimu angeweza kuwaauliza pahali wanapolala, madhara ya wadudu hawa, kama kuna faida za kuwa na wadudu hawa, maumbile yao na mengine yahusuyo wadudu. Maswali yalipojibiwa, mwalimu hakuwasitisiza wanafunzi watoe majibu kwa kutumia sentensi kamili bali aliwaachia tu wajibu “ndio” “panzi” “zenengo” “ watu”. Mwalimu angeweza kuwahimiza ili waweze kujibu “ndio, tumewaona”. Kwa namna walimu walivyoauliza wanafunzi maswali, wasingeweza kukuza stadi ya mazungumzo kwa upana katika ziara yao kwa sababu hakuwapa fursa hiyo. Hivyo, wanafunzi hawatakuwa na umilisi mzuri wa kutumia lugha.

Matokeo ya mahojiano kati ya mtafiti na walimu yalionesha kuwa asilimia 9% (16) walikubali kuwa watoto wanapenda sana kitendo cha kwenda ziara. Aidha walimu walikubali kuwa watoto wanapenda kuzungumzia mambo waliyoyaona, kuchora picha za vitu mbalimbali walivyoviona na kueleza mambo na vitu walivyoviona huko ziarani. Misamiati mipya na matumizi ya lugha, pia hupata ufahamu wa kanuni za lugha. Mwalimu wa Star anaeleza;

“Sisi kila ifikapo mwisho wa mwaka wa masomo huwa tunafanya ziara na watoto wetu katika sehemu tulioichagua. Tunapokuwa kwenye matembezi, watoto huchunguza na kuuliza maswali kutaka kujua vitu vingi, nasi tunawajibu. Nasi pia huwa tunawajibu. Hapo watoto huwa tunawafundisha maneno mapya kutokana na mambo waliyoyaona, ila, ziara inapoteza muda na ina gharama ndio maana njia hii hatuitumii sana”.

TIE (2003) inaeleza kuwa, njia ya ziara na uchunguzi huwawezesha watoto kutembelea mahali na kufanya uchunguzi kwa wakati mmoja. Njia hii huwasaidia watoto kuwa wadadisi, kwani wanapokwenda kwenye ziara huona na kuchunguza vitu vy aina mbalimbali. Watoto huuliza maswali na pia hujadiliana juu ya mambo wanayoyaona. Hivyo basi, watoto hawa hujifunza maneno mapya ambayo baadaye huyatumia katika maisha yao ya kila siku.

Kutokana na matokeo ya data pamoja na hoja hizo, tunaweza kusema kwamba kushindwa kwa wanafunzi wa shule za awali kumudu vyema stadi ya mazungumzo, kunatokana na walimu walio wengi kushindwa kuongoza vyema mazungumzo katika ufundishaji wa stadi hii. Sababu kubwa ni baadhi ya walimu kutokuwa na utaalamu wa

kuendeleza vitendo vya kufanya baada ya ziara na uchunguzi, pamoja nakushindwa kuendeleza mazungumzo yanayotokana na mambo yaliyo katika jamii yao.

4.2.7 Njia ya Bungua Bongo katika Ufundishaji Stadi Yya Mazungumzo kwa Watoto.

Mtafiti alifanya mahojiano na walimu kutaka kujuu kama wanatumia njia ya bungua bongo kufundishia watoto stadi ya mazungumzo. Matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha kuwa asilimia 12.5% (7) ya walimu waliohojiwa wanafundisha stadi hiyo kwa njia ya bungua bongo.

Kwa upande mwingine asilimia 3.5% (7) ya walimu walishuhudiwa darasani wakifundisha watoto stadi hii kwa njia ya bungua bongo. Walimu walipotazamwa darasani, matokeo yameonyesha kuwa walimu hawaitumii njia hii ipasavyo hivyo wanasababisha wanafunzi wasiweze kujieleza kwa kuzungumza. Aidha, idadi kubwa ya walimu (96.4%) waliotazamwa wakifundisha darasani hawakutumia njia hii kufundisha stadi ya mazungumzo. Si hayo tu, lakini pia idadi kubwa (87.5%) ya walimu waliohojiwa hawakutumia njia hii kufundisha stadi ya mazungumzo.

Aidha walimu waliotazamwa wakitumia njia hii katika ufundishaji, hawakutoa fursa sana kwa wanafunzi kujieleza. Walimu waliuliza maswali baadae wao ndio walitawala katika mazungumzo na kusababisha watoto wachache tu wazungumze, hivyo wanadumaza matumizi ya lugha ya mazungumzo kwa watoto.

ZMRC (2000) inaeleza kuwa njia ya bungua bongo hutumia kwa kuibua fikra za watoto. Mwalimu anaweza kuibua fikra za watoto kwa kutumia maswali ya wazi. Fikra hizo wanazieleza kwa kutumia uzoefu wao katika mazingira wanayoishi. ZMRC imeendelea kueleza kuwa, njia hii pia hutumika katika kufafanua dhana mbalimbali wakati somo linaendelea hivyo watoto hupata fursa ya kuzungumza kwa kutoa mawazo yao kwa haraka. Lugha hutumiwa kwa kufikiri, hivyo watoto wanapofikiri na kutumia lugha huweza kuunganisha mawazo yao.

Kutokana na matokeo ya data pamoja na hoja hizo, tunaweza kusema kwamba kushindwa kwa wanafunzi wa shule za awali kumudu vyema stadi ya mazungumzo. Walimu wengi hushindwa kutumia vyema njia ya bungua bongo katika ufundishaji wa stadi hii , hivyo hawatoi fursa nzuri kwa watoto katika kukuza matumizi ya lugha. Sababu kubwa ni walimu hawa wanatoa nafasi kwa watoto wachache ambao tayari wamejengeka vizuri katika stadi ya mazungumzo na kuwaacha wale ambao hawana umahiri mzuri wa kuzungumza na kusababisha watoto hawa kushindwa kumudu stadi ya mazungumzo. Aidha walimu wachache sana ndio hutumia njia hii kuwfundisha wanafunzi stadi hii, hivyo wanafunzi wachache tu ndio hupata fursa ya kujifunza stadi hii ya mazungumzo.

4.2.8 Njia ya Vitendawili katika Kufundishia Stadi ya Mazungumzo kwa Watoto

Mtafiti alitumia mbinu ya mahojiano kuwahoji walimu kama wanafundisha stadi ya mazungumzo kwa njia ya vitendawili. Matokeo ya utafiti huu kwa njia hii yalionesha kwamba asilimia 100% (56) wanatumia njia ya vitendawili kufundisha stadi ya mazungumzo.

Kwa upande mwingine walimu walioshuhudiwa darasani wakifundisha, matokeo yalionesha kwamba asilimia 57% (32) ya walimu ndio wanafundisha watoto stadi ya mazungumzo kwa njia ya vitendawili. Kutokana na matokeo ya data, tunaweza kusema kuwa ufundishaji wa stadi ya mazungumzo kwa njia ya vitendawili hausaidii wanafunzi wengi kukuza stadi ya mazungumzo kutokana na fursa chache wanazopata wanafunzi kulikosababishwa walimu.

Katika shule zote zilizotembelewa na mtafiti alishuhudia njia hii ya kufundishia stadi ya mazungumzo ikifurahiwa sana na wanafunzi, ingawaje wanafunzi waliopata fursa ya kutega na kutegua vitendawili walikuwa ni wachache. Walimu walishindwa kufafanua maana ya baadhi ya maneno pia kuweka sawa miundo ya sentensi zilizokosewa na watoto.

TIE (2003) inaeleza kuwa, vitendawili pamoja na kuburudisha watoto, pia hujenga uwezo wa udadisi kwa watoto hivyo husaidia kukuza stadi wa mazungumzo hasa kwa watoto wadogo. Vitendawili husaidia wanafunzi kukuza lugha yao. Wanapotega na kutegua vitendawili, wanafunzi wanajifunza maneno mapya, maana ya maneno hayo na matumizi ya maneno hayo katika jamii yao.

4.3 Mahojiano na Walimu Wakuu kuhusu Ufundishaji wa Stadi ya Mazungumzo.

Mtafiti alitumia mbinu ya mahojiano kuwahoji walimu wakuu kama wanaendesha mafunzo ya ndani kwa walimu kuhusu ufundishaji wa stadi ya mazungumzo. Matokeo ya mahojiano hayo yalionesha kwamba asilimia 100% (20) ya walimu wakuu walikiri kuwa hawana uwezo wa kitaalamu kuhusu ufundishaji wa stadi ya mazungumzo. Aidha

walidai kuwa, hawana mitandao ya kompyuta ambayo itawasaidia walimu kujitafutia maarifa ya kuweza kukuza uelewa wa namna ya kufundisha lugha hasa stadi ya mazungumzo

Kutokana na matokeo ya hoja hizo, tunaweza kusema kwamba kushindwa kwa wanafunzi wa shule za awali kumudu vyema stadi ya mazungumzo, kunatokana na walimu wakuu kushindwa kutoa mafunzo kwa walimu juu ya ufundishaji wa stadi hii. Sababu kubwa ni kutokuwa na utaalamu wa kutosha wa ufundishaji wa lugha ya mazungumzo, ingawaje miutasari imeelekeza njia za ufundishaji wa stadi ya mazungumzo.

4.4 Mahojiano na Wakaguzi wa Elimu ya Awali na Mratibu Wa Kituo Cha

Walimu

Mtafiti alitumia mbinu ya mahojiano kumuhoji mratibu wa kituo cha walimu na wakaguzi wa somo la Kiswahili kwa madarasa ya elimu ya awali, kama wanaendesha mafunzo kwa walimu kuhusu ufundishaji wa stadi ya mazungumzo. Matokeo ya mahojiano hayo yalionesha kwamba asilimia 100% (3) walikiri kuwa hawajafanya mafunzo kuhusu ufundishaji wa stadi ya mazungumzo. Aidha walidai kuwa kulifanyika mafunzo ya siku mbili kwa baadhi ya walimu wa shule za serikali. Mafunzo hayo yalihusu njia za kufundishia kwa jumla.

Matokeo ya utafiti yameonyesha kuwa, walimu hawapewi mafunzo yahayohusiana na ufundishaji wa stadi ya mazungumzo, hivyo tunadiriki kusema kuwa ni sababu

mojawapo ya wanafunzi kushindwa kumudu stadi ya mazungumzo kwa walimu hawana ujuzi wa kutosha juu ya njia za kufundisha stadi ya mazungumzo.

4.5 Zana Za Kufundishia Na Kujifunzia Stadi Ya Mazungumzo

Mtafiti alitumia mbinu ya mahojiano kuwahoji walimu kama wanafundisha stadi ya mazungumzo kwa kutumia zana za kufundishia ili wanafunzi waelewe matumizi ya lugha ipasavyo. Matokeo ya utafiti huu kwa njia hii yalionesha kwamba asilimia 96% (54) wanatumia zana za kufundishia wanafunzi stadi ya mazungumzo.

Vilevile, matokeo ya utafiti huu kuhusu walimu walioshuhudiwa darasani wakifundisha, yalionesha kwamba asilimia 21% (12) ya walimu ndio walifundisha wanafunzi stadi ya mazungumzo kwa kutumia zana za kufundishia kama picha zilizochorwa, wanasesere, vitabu vya picha na hadithi na vitu halisi wakati wa kusimulia hadithi na kutega vitendawili. Zana hizi ziliwasaidia wanafunzi kwa kiasi kuelewa misamiati mipy, kuunda maneno na kutunga sentensi ndogo ndogo.

ZMRC (2010) inaeleza kuwa mwalimu anapotoa hadithi kwa kutumia zana, watoto wanafurahia lugha na kujifunza mambo mapya na maneno mapya pia. Watoto huuliza maswali yanayotokana na hadithi na pia hutaka kuelewa zaidi juu ya picha zilizomo kwenye hadithi na hivyo hukuza stadi yao ya mazungumzo.

Matokeo ya majibu ya mahojiano na walimu na yale ya ushuhudiaji yana tofauti kubwa sana. Wakati matokeo ya mahojiano yalionyesha kuwa walimu wengi (96%) wanatumia

zana za kufundishia, ushahidi wa ushuhudiaji ulionyesha kuwa walimu wachache (21%) tu ndio wanatumia zana za kufundishia stadi hii.

Kwa kuwa walioshuhudiwa kutumia zana za kufundishia stadi hii ni wachache sana, basi tunaweza kusema kuwa idadi ya wanafunzi wanaojifunza stadi hii kutohuna na walimu kutumia zana za kufundishia ni wachache sana. Hivyo wanafunzi walio wengi hushindwa kupata vema stadi ya mazungumzo kuitia mafundisho ya shuleni.

Jedwali na 3: Zana wanazotumia walimu kufundishia stadi ya mazungumzo ambavyo vimeonekana darasani na mtatiti

AINA YA ZANA	MIFANO YA ZANA
Zana zinazotoa sauti	Redio
Vitu halisi	Nguo, chupa, makopo, vitabu vyatya, maua, Mbegu za aina tofauti, magazeti.
Vifani	Wanasesere kama magari, watoto bandia, mipira, boksi la sinema na vitu vingi ambavyo watoto wanachezea
Michoro na picha	Machati, vipeperushi, mabango, kadi za kusomea zenye michoro na picha.

Chanzo: Utafiti wa uwandani 2015

Walimu walishuhudiwa kutumia zana hizi za kufundishia walipokuwa wakifundisha kwa njia ya kusimulia hadithi, kutega vitendawili pamoja na maswali na majibu.

4.6 Mahojiano na Wakaguzi na Mratibu wa Elimu ya awali Kuhusu Zana za Kufundishia Stadi ya Mazungumzo

Mtafiti alitumia mbinu ya mahojiano kuwahoji wakaguzi na mratibu wa elimu ya awali kama walimu wanafundisha stadi ya mazungumzo kwa kutumia zana za kufundishia. Matokeo ya utafiti huu yalionesha kwamba asilimia 100% (3) wamekubali kuwa walimu wanatumia zana kufundishia stadi ya mazungumzo.

Matokeo ya utafiti yalionesha kuwa wakaguzi wote wawili na mratibu wa kituo cha walimu wamekubali kuwa zana za kufundishia ndizo zinazomvutia mtoto kuweza kujifunza. Aidha, wakaguzi walidai kuwa kila wanapokwenda uwandani kukagua walimu, huwa wanaangalia uwepo wa zana pamoja na matumizi ya zana hizo kwa watoto na walimu wakati wa ufundishaji kwa jumla na sio katika kukuza stadi ya mazungumzo pekee.

Tassoni (2002) anaeleza kuwa, mwalimu akitumia zana ipasavyo katika ufundishaji wa stadi ya mazungumzo, watoto hukuza stadi hii ka haraka kwani hufurahia sana kuzungumza wenyewe kwa wenyewe kuhusiana na zana walizopewa na mwalimu.

Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa matumizi ya zana za kufundishia katika ufundishaji wa stadi ya mazungumzo, haujatiliwa mkazo ipasavyo na wakaguzi wa somo la lugha ya Kiswahili katika ngazi ya elimu ya awali. Walimu wanashindwa kutumia zana za kufundishia katika kuwashimiza wanafunzi kueleza maana ya picha

wanazoziona, kutunga sentenzi ndogo, kutaja silabi za neno. Hivyo wanafunzi hawajifunzi vizuri stadi hii na kupelekea kushindwa kujieleza.

4.7 Changamoto Wanazokabiliana Nazo Walimu Katika Ufundishaji Wa Stadi Ya Mazungumzo

Mtafiti alitumia mbinu ya mahojiano kuwahoji walimu kama kuna changamoto wanazokabiliana nazo katika kufundisha stadi ya mazungumzo. Matokeo ya utafiti huu yalionesha kwamba asilimia 100% (56) wamekubali kuwa kuna changamoto katika ufundishaji stadi ya mazungumzo.

Aidha, walimu asilimia 21% (12) walioshuhudiwa darasani wakikabiliana na changamoto ya matumizi ya maneno ya lahaja ya Kipemba ambayo hayakutolewa ufafanuzi wake, hivyo kuwanyima watoto fursa ya kukuza stadi ya mazungumzo.

Mtafiti pia alitumia mbinu ya mahojiano kuwahoji wakaguzi wa somo la Kiswahili katika madarasa ya elimu ya awali, pamoja na mratibu wa kituo cha walimu wa elimu ya awali kuhusu changamoto wanazokabiliana nazo walimu katika ufundishaji wa stadi ya mazunguzo. Matokeo ya utafiti yalionesha kuwa wakaguzi pamoja na mratibu wa kituo cha walimu wamekubali kuwa kuna changamoto wanazokabiliana nazo walimu katika ufundishaji wa stadi ya mazungumzo. Baadhi ya changamoto zilizoainishwa ni pamoja na matumizi sahihi ya njia za kufundishi stadi yamazungumzo Aidha, wakaguzi hao walieleza kuwa, hakuna mafunzo yaliyotolewa kwa walimu wa shule za awali kuhusiana na ufundishaji wa stadi ya mazungumzo kutokana na ukosefu wa fedha za kuendeshea mafunzo.

Tassoni (2002) anaeleza kuwa, walimu kutoweza kupanga vitendo vyta ufundishaji wakati wa ufundishaji wa stadi ya mazungumzo, pia kutokuwa na mbinu za kuendeleza mazungumzo ya watoto ni changamoto kubwa wanazokabiliana nazo walimu. Tassoni ameendelea kueleza kuwa, walimu wanakosa stadi za kuauliza wanafunzi maswali ya wazi ambayo kwa kawaida hutoa fursa ya mazungumzo.

Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa changamoto wanazokabiliana nazo walimu katika ufundishaji wa stadi ya mazungumzo ikiwemo njia za kufundishia stadi hiyo, hazijashughulikiwa ipasavyo na wakaguzi wa somo la lugha ya Kiswahili katika ngazi ya elimu ya awali. Walimu hawajapewa mafunzo ya kutosha ya ufundishaji wa stadi hii, hivyo wanashindwa kuwafundisha veme wanafunzi wao stadi ya mazungumzo. Kwa sababu hiyo, wanafunzi wanashindwa kujieleza vema.

4.8 Muhutasari

Katika sura hii matokeo ya data, uwasilishaji wa data na matokeo yake zimewasilishwa. Matokeo hayo yalihusu njia mbalimbali za kufundishia stadi ya mazungumzo shulenii baada kufanya mahojiano na walimu pamoja na ushuhudiaji uliofanyika madarasani. Sura hii pia imewasilisha zana zilizotumiwa na walimu katika ufundishaji wa stadi ya mazungumzo zilizoshuhudiwa darasani wakati wa tendo la ufundishaji pamoja na zile zilizotajwa na walimu wakati wa mahojiano. Pia, changamoto wanazokabiliana nazo walimu katika ufundishaji wa stadi ya mazungumzo zimeelezwa kwa njia ya majadiliano. Aidha, wakaguzi wa somo la kiswahili na mratibu wa kituo cha elimu ya awali waliohojiwa walikubali kuwa walimu wana mapungufu katika matumizi ya njia za

kufundishia pamoja na matumizi ya zana za kufundishia stadi ya mazungumzo. Aidha, utafiti umejadili maana ya viashiria vya matokeo hayo.

Matokeo hayo yameonyesha kwa jumla kwamba walimu walio wengi hawatumii njia mbalimbali za kufundishia stadi hii na wala hawatumii zana za kufundishia kama zilivyopendekezwa na wataalamu.

Aidha, matokeo hayo yamedhihirisha kuwa walimu hawana ujuzi wa kutosha juu ya ufundishaji wa stadi hii. Hii imetokana na hali ya walimu kukosa mafunzo kazini ambayo yangewasaidia kuboresha ufundishaji wa stadi ya mazungumzo. Hii imetokana na ukweli kuwa wakaguzi na washauri wa elimu ya awali kutopita kwenye vituo hivi hasa katika shule za jamii na za binafsi. Hii ni kurudisha nyuma ufundishaji wa stadi ya mazungumzo.

Kwa hiyo, walimu kushindwa kufundisha kwa ufanisi stadi hii ya mazungumzo kutokana na kukosa umahiri na ujuzi wa kutosha juu ya njia za kufundishia stadi hii, kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusiana matumizi ya zana za kufundishia pamoja na kushindwa kukabiliana na changamoto wanazokutana nazo wakati wa ufundishaji wa stadi ya mazungumzo.

Jedwali no 3: Njia wanazotumia walimu katika ufundishaji wa stadi ya mazungumzo

Aina ya njia ya kufundishia	Walimu walioitaja kuwa wanaitumia njia hii	Walimu walioshuhudiwa wakitumia njia hii
Majadiliano	17 (30.3%)	24 (42.8%)
Maswali na majibu	56 (100%)	56 (100%)
Hadithi/masimulizi	54 (96%)	12 (21%)
Maigizo	05 (9%)	01 (1.7%)
Michezo na nyimbo	56 (100%)	24 (43%)
Ziara na uchunguzi	05 (09%)	01 (1.7%)
Bungua bongo	07 (12.5%)	02 (3.5%)
Vitendawili	56 (100%)	32 (57%)

Chanzo: Utafiti wa uwandani 2015.

SURA YA TANO

5.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1.Utangulizi

Utafiti huu umechunguza uhusiano uliopo baina ufundishaji wa stadi ya mazungumzo kwa wanafunzi wa shule za awali na kukwama kwao kupata maarifa ya kutosha ya stadi hiyo. Utafiti huu ulifanyika wilaya ya Chake Chake, mkoa wa Kusini, Pemba. Jumla ya shule ishirini zikiwemo za serikali za binafsi na za jamii zilishiriki katika utafiti huu.

5.2 Hitimisho

Katika uchambuzi wa data, matokeo ya utafiti yameonyesha kuwa, walimu hawapewi mafunzo yahusuyo ufundishaji wa stadi ya mazungumzo. Hii ni sababu mojawapo ya wanafunzi kushindwa kumudu stadi ya mazungumzo kwa kuwa walimu hawana ujuzi wa kutosha juu ya njia za kufundisha stadi ya mazungumzo.

Matokeo ya utafiti pia yanaonyesha kuwa, walimu hawana ujuzi wa kutosha wa matumizi ya zana za kufundishia katika ufundishaji wa stadi ya mazungumzo. Walimu wanashindwa kutumia zana za kufundishia katika kuwashimiza wanafunzi waitumie lughaya mazungumzo kwa kuwafundisha misamiati, sentensi, maana ya maneno pamoja na matumizi mingine ya lugha.

Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa changamoto wanazokabiliana nazo walimu katika ufundishaji wa stadi ya mazungumzo ikiwemo njia za kufundishia stadi hiyo, hazijashughulikiwa ipasavyo na wakaguzi wa somo la lugha ya Kiswahili katika ngazi ya elimu ya awali. Walimu hawajapewa mafunzo ya kutosha ya ufundishaji wa stadi hii,

hivyo wanashindwa kuwafundisha vema wanafunzi stadi ya mazungumzo. Kwa sababu hiyo, wanafunzi wanashindwa kujieleza vema.

5.3 Mapendekezo

Ili stadi ya mazungumzo iweze kufundishwa kwa ufanisi, kituo cha walimu kitoe mafunzo kwa walimu wa lugha ya Kiswahili juu ya kutumia njia anuai za kufundishia stadi ya mazungumzo. Walimu waelekezwe namna bora ya kutumia zana za kufundishia lughai ya mazungumzo na kuwasaidia jinsi ya kukuza stadi hii kwa wanafunzi. Aidha, wakaguzi wanaokagua katika madarasa ya elimu ya awali wanapokagua ufundishaji wa lugha ya Kiswahili, wakague pia ufundishaji wa stadi ya mazungumzo ili waweze kushauriana na walimu pale ambapo watagundua kuna changamoto.

Walimu wakuu wawasisitiza walimu wa lugha ya Kiswahili kutafuta maarifa ya ziada katika maktaba za skuli, maktaba za wilaya na kwenye mitandao ili waelewe namna bora ya ufundishaji wa stadi ya mazungumzo ili wanafunzi waweze kutumia lugha yao ipasavyo.

Walimu wajenge utamaduni wa kujisomea na kutafuta maarifa ya ziada yanayohusu ufundishaji wa stadi ya mazungumzo badala ya kusubiri mafunzo yanayoandaliwa na wizara ya elimu. Serikali na wakuza mitaala ya elimu waandae vitabu vya kiada pamoja na vitabu vya ziada vitakavyowasaidia walimu katika ufundishaji wa stadi ya mazungumzo. Aidha, waandae mafunzo maalumu kwa walimu kuhusu ufundishaji wa stadi ya mazungumzo ili walimu waweze kufundisha kwa ufanisi.

Utafiti kama huu ufanyike katika sehemu nyingine za Zanzibar, Tanzania na hata nje ya nchi ili kuona ufundishaji wa stadi ya mazungumzo katika sehemu tofauti. Aidha, utafiti huu pia ufanyike katika viwango vyengine vya elimu yaani darasa la kwanza hadi ngazi ya chuo kikuu ili kuweza kusaidia kukuza stadi ya maungumzo.

Tafiti nyingine zinazohusu stadi ya kusikiliza, kusoma na kuandika katika viwango tofauti vya elimu, kuanzia elimu ya awali hadi vyuo vikuu zifanyike ili kukuza ufanisi katika ufundishaji wa stadi hizi.

Tathmini ya ufundishaji wa stadi ya mazungumzo katika ngazi ya elimu ya awali na viwango vyengine vya elimu, pamoja na tathmini ya stadi za kusikiliza, kusoma na kuandika zifznyike ili kuona ufanisi wa ufundishaji wa stadi hizi pamoja na changamoto zake.

MAREJEO

- 21st Century Basic Education Program TZ21; (2010), Ufundishaji wa Kusoma, DSM.
- Abbass, A. (2011), A survey in Teaching Strategies in ESL Classroom, PhD Linguistics, Research Scholar, www.languageinindia.com.
- Adam, J. na Kamuzora, F. (2008), Research Methods for Business and Social
- Andrews, R. (2003), Research Question, Continuum, London.
- Anning, A. (2009), Early Childhood Education : Society and Culture,
- Arshad, N. (2014), Class Activities for Developing speaking Skills, Linkedin Corporation.
- Baker, J. (2003), The English Language Teachers Handbook, Continuum. London.
- Beaver, M. (2004), Early Years Care and Education, Nelson Thorns Ltd.
- Beck, D. (2015), Linkedin Corporation, 12.2.2015, 12:15
- Billows. D; (1966), The Techniques of Language Teaching, Longmans, London.
- Bruce, T. (2005), Early Childhood Education, Hodder Education, London.
- Bruce, T. and Maggitt. C. (2006), Child Care and Education, Hodder Education.
- Burkart, G. (1998), Spoken Language: What is and How to Teach It, Modules for Childhood Development, MRC East Africa. Mombasa, Kenya.
- Cohen, L. (2007), Research Methods in Education, Routledge ,
- Dr. Shrouf, F. (2014), Teaching and Improving Speaking Skill, Philadelphia University.
- Education, Zanzibar.
- Educational Publishers, London.
- Goodman, K. (1976), Language and Thinking in School, Richard Publishers. USA.
- Intihar, N. (2006) Developing Speaking Skills in the Young Learners Classroom,
- Kayi, H. (2006), Teaching Speaking Activities to Promote speaking in a Second
- King'ei, K. (2010), Misingi ya Isimujami,. TATAKI, Dar es Salaam.
- Kothari, C. (2003), Research Methodology – Methods and Techniques (2nd Ed)

- Language, University of Nevada. USA.
London.
- Lyons, J. (1981), Language and Linguistics. An Introduction. Cambridge
- Massamba, D. (2004), Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha, TUKI, Dae es Salaam.
- Mdee, S. (2014), Lugha katika jamii, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Meggitt, C. (2000), Child Development, An Illustrated guide, Heinemann
- Meggitt, C. (2008), Child Care and Education, Hodder Education, London.
- Mekacha, R. (2011), Isimijamii: Nadharia na Muktadha wa Kiswahili, TATAKI..
- MFL, (2011), Speaking Skills Teaching Resource, TES Connect. 09.2.2015, 11:06.
- Ministry of Education Zanzibar; (2006), Zanzibar Education Policy, Ministry of
- Mmallavi, A. (1977), Lugha Katika Jamii, East African Publishing House, DSM.
- Msanjila, Y; (2009), Isimujamii Sekondari na Vyuo, TUKI, Dar es Salaam.
- Mtana, N. (2003), Ufundishaji Unaozingatia Ujenzu wa Maan,. Wizara ya Elimu Na Utamaduni, Dar es Salaam.
- New Delhi, K.K. Gupta for New Age International (P) Ltd.
- New York.USA
- O'hara, M. (2004), Teaching 3 – 8, Continuum, London.
- Oradee, T. (2012) Developing Speaking Skills Using Three Communicative Activities.
- Oseno, B. (2014) Teaching Speaking Skills: Challenges of Using Integrated Approach in Secondary Schools. (pdf)
- Palmer, F. (1976), Semantics, Cambrige University Press.
- Proffessional Preparation for Teaching Assistance in Foreign Language,
SAGE Publications Ltd.
- Studies, Mzumbe Book Project.
- Tassoni, P na Hucker. K; (2000), Planning Play and the Early Years, Heinemann Educational Publishers, Oxford.

Tassoni, P. (2004), Diploma in Pre-school Practice, Heinemann, UK.

The Elimu Network. (saa 8:07 mchana (15.12.2014).

The Internet TESL Journal. Vol X11 no 11. <http://teslj.org> 12.2.2015, 1:12.

The National Capital Resource Centre. (saa 2:20 usiku 15.12.2014)

United Kingdom.

University Press. London.

Washington DC. Centre for Applied Linguistics.

Wizara ya Elimu na Utamaduni; (1996), Ufundishaji wa Kiswahili, Wizara ya Elimu Na Utamaduni, Dar es Salaam.

Wizara ya Elimu na Utamaduni; (1996), Zana za Kufundishia na Kujifunzia, Wizara ya Elimu Na Utamaduni, Dar es Salaam.

Yule. G; (1997). The Study of Language. University Press, Cambridge.

Zanzibar Madrasa Resouce Centre; (2000), Pre School Curriculum, MRC East African Regional Office, Mombasa, Kenya.

Zanzibar Madrasa Resource Centre; (2010), Pre School Curriculum, Supporting Early

VIAMBATANISHO

KIAMBATISHO I

RATIBA YA KUFANYA UTAFITI MPANGO WA KAZI 2014 -2015

KIAMBATISHO II**BAJETI YA KAZI YA UTAFITI**

	MAELEZO	GHARAMA
1	Matayarisho ya uandishi wa pendekezo - Vifaa vya kuandikia k.v madaftari, kalamu, rula - Huduma za komputa - Huduma za intaneti - Gharama za usafiri kwa ajili ya kukutana na wadau - Usafiri kwa ajili ya kupitia kazi tangulizi	50,000/ 200,000/ 50,000/ 100,000/ 20,000/
2	Matayarisho ya zana za kukusanya data - Kutayarisha masuali ya usaili - Kuandaa zana za kurikodia wakati wa ushuhudiaji	10,000/ 40,000/
3	Kukusanya data - Usafiri kwa ajili ya kufuata watafitiwa - Usafiri wa kwenda maktaba ya taifa	30,000/ 10,000/
4	Uchambuzi wa data	150,000/
5	Uandishi wa ripoti	100,000/
6	Usafiri wa kuwasilisha ripoti jijini Dar es Salaam	300,000/
7	Kuchapa na kutoa ripoti.	250,000/
8	JUMLA KUU	1,310,000/

KIAMBATISHO III**ORODHAHAKIKI YA UCHUNGUZI WA UFUNDISHAJI WA STADI YA MAZUNGUMZO DARASANI KWA WALIMU.****Jina la mwalimu.....****Jina la shule.....****Darasa.....****Tarehe.....**

**Alama 1. Kiwango kidogo/hapana 2. Kipengele hiki kinafanyiwa kazi kiasi
3.kipengele hiki kinafanyiwa kazi vizuri 4. Utekelezaji wa ufanisi wa hali ya juu
kabisa.**

	1	2	3	4
NJIA ZA KUFUNDISHIA				
Uteuzi wa njia kwa mujibu wa mada				
Umahiri wa matumizi ya njia				
Njia iliyoteuliwa inawafanya watoto waweze kuzungumza				
Mwalimu aliwashirikisha watoto ipasavyo				
Mwalimu alianisha misamiati mipyä kwa watoto				
Watoto wasiopenda kuzungumza waliwasaidia wazungumze				
Watoto wenyе ulemavu wa ala za sauti (kama wapo) walisaidiwa				
Mwalimu aliwataka watoto kuimba nyimbo au kusimulia hadithi				
Mwalimu amerekebisha matamshi watoto walipokosea				
ZANA ZA KUFUNDISHIA				
Zana zilizotumika ziliikuwa za kutosha				
Watoto walipata fursa ya kutumia zana				
Mwalimu aliuliza maswali ya wazi ili watoto wazungumze				
Mwalimu aliwahimiza watoto waulize maswali kuhusiana na matumizi ya zana				
Watoto wenyе ulemavu (kama wapo) walipatiwa zana kulingana na mahitaji yao				
Machati na vipeperushi vimebandikwa kwenye kuta				
Vitabu vyा hadithi na picha viro ndani ya darasa				
Watoto wanavitumia vitabu na picha kwa kuzungumza pamoja				
CHANGAMOTO : Namna walimu wanavyozikabili				

KIAMBATISHO IV

MASWALI YA USAILI KWA WALIMU WA SHULE ZA AWALI JUU YA UFUNDISHAJI WA STADI YA MAZUNGUMZO

1. UTAMBULISHO
2. Una muda gani sasa tangu ufundishe Kiswahili katika madarasa ya awali?
3. Unatumia muhutasari wa shule za serikali au mwengine? (kwa wale wa shule za jamii na za binafsi)
4. Muhutasari wako unaotumia umeainisha ufundishaji wa stadi ya mazungumzo?
5. Njia gani unatumia katika kufundisha stadi ya mazungumzo?
6. Tafadhalii naomba nieleze kwa ufupi unafundishaje kwa kutumia njia hizi.
(angalau njia tatu)
7. Ni zana gani unatumia kwa kufundishia stadi ya mazungumzo?
8. Unavitumiaje zana hivi kwa kufundishia stadi ya mazungumzo?
9. Ni changamoto gani unakutana nazo katika ufundishaji wa stadi ya mazungumzo?
10. Kama zipo, changamoto hizi unakabiliana nazo vipi?
11. Kama una mtoto mwenye ulemavu wa ala za sauti unamsaidiaje?
12. Kuna mafunzo yoyote uliyopata yanayohusiana na ufundishaji wa stadi ya mazungumzo? Kama yapo yalikuwa yanahu nini na yalitolewa lini.
13. Washauri wa vituo vya walimu huwa wanawashauri nini kuhusiana na ufundishaji wa stadi ya mazungumzo katika lugha ya Kiswahili?
14. Unadhani ni muhimu kupatiwa mafunzo juu ya ufundishaji wa stadi hii kama ndio au hapana, toa sababu.
15. Unapokuwa na tatizo kuhusiana na ufundishaji nwa stadi hii unafanyaje?
16. Una maandiko yoyote ya rejea yanayohusiana na stadi hii?
17. Toa maoni yako kuhusiana na ufundishaji wa stadi ya mazungumzo.

SHUKRANI KWA KUTUMIA MUDA WAKO

KIAMBATISHO V.**MASWALI YA USAILI KWA WAKAGUZI WA ELIMU YA AWALI**

1. UTAMBULISHO
2. Una muda gani sasa tangu uanze kukagua walimu wa elimu ya awali?
3. Mnapoangalia ufundishaji wa lugha ya Kiswahili kwa walimu wa elimu ya awali huwa mnaangalia na ufundishaji wa stadi mazungumzo?
4. Kama ndio, ni mambo gani hasa ambayo mnayaangalia?
5. Mnatoa ushauri gani kwa walimu ambao hawafundishi vema stadi za ufundishaji wa lugha ya mazungumzo?
6. Katika fomu yenu ya tathmini kuna kipengele cha matumizi ya zana katika kufundisha stadi ya mazungumzo?
7. Inapotokea kwenye ukaguzi na mkagundua kuwa walimu wana matatizo katika ufundishaji wa stadi ya mazungumzo mnafanyaje?
8. Toa maoni yako kuhusiana na ufundishaji wa stadi ya mazungumzo.

SHUKRANI KWA KUTUMIA MUDA WAKO

KIAMBATISHO VI**MASWALI KWA MRATIBU WA KITUO CHA WALIMU**

1. UTAMBULISHO
2. Mnapoangalia ufundishaji wa lugha ya Kiswahili kwa walimu wa elimu ya awali huwa mnaangalia na ufundishaji wa stadi mazungumzo?
3. Kama ndio, ni mambo gani hasa ambayo mnayaangalia?
4. Mnawasaidiaje walimu katika ufundishaji wa stadi hii?
5. Kuna mafunzo yatoleawayo kituoni kwa ajili ya walimu kuhusu utumiaji wa stadi pendekezwa za ufundishaji wa lugha ya mazungumzo?
6. Walimu wanakuja katika kituo kuulizia ama kujisomea mambo yanayohusu ufundishaji wa stadi ya mazungumzo?
7. Mnawafutilia walimu kuona ufundishaji unavyofanyika?
8. Jitihada gani zinafanywa na kituo ili kuona stadi pendekezwa za ufundishaji lugha ya mazungumzo zinafuatwa na walimu.
9. Maoni yako kuhusiana na ufundishaji wa stadi hii.

SHUKRANI KWA KUTUMIA MUDA WAKO

KIAMBATISHO VII

06/03/2015

THE OFFICER IN-CHARGE
MINISTRY OF EDUCATION AND VOCATIONAL TRAINING
PEMBA

RE: MRS. LAILA HEMED ALI REG/NO. PG 201404035

The Open University of Tanzania is a full flagged University established by an Act of Parliament No. 17 of 1992. The university offers various programs on Open and distance learning (ODL) mode with centers throughout the country.

Therefore, On behalf of our university, I am pleased to inform you that, the bearer of this letter is our student at Open University of Tanzania. She is pursuing Master of Art in Kiswahili. She is now on a process of undertaking her research with title: **UFUNDISHAJI WA STADI YA MAZUNGUMZO KATIKA SHULE ZAWALI**

In order for her to complete of her study successfully, she must visit pre-schools in Chake Chake District.

Kindly accord Mrs. Laila Hemed Ali permission to visit these schools.

Thank you for your usual support.

JUMA R. KHAMIS

DIRECTOR

KI
THE OPEN UNIVERSITY OF TANZANIA
PEMBA CENTER

OFISI YA WIZARA YA ELIMU,
NA MAFUNZO YA AMALI,
PEMBA.

13 / 03 / 2015

REF.NO..... *EFP/P/132/8/88*